
SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Serikali** kuvipa masharti magumu vituo vya mafuta vilivyojengwa kiholela

UKURASA 2




UKURASA 11

Nipashe
Jumatatu Septemba 13, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580702
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# SAMIA AFYEKA MAWAZIRI

UKURASA 8



Rais Samia Suluhu Hassan

## 'IN'



Stergomena Tax



Ashatu Kijaji



January Makamba



Makame Mbarawa

## 'OUT'



Merdad Kalemani



Leonald Chamuriho



Faustine Ndugulile

## MWANASHERIA MKUU



Eliezer Feleshi

## Kauli ya Ndugai safari za mawaziri Dar yaibua wadau

UKURASA 3

# Mkakati waja kuwapa wengi chanjo corona

UKURASA 2



MICHEZO
IBRAHIMOVIC: MIMI NI ZAIDI YA MESSI, RONALDO UK.21
MAONI, KATUNI UK.6

# Wakulima wa mpakani watahadharisha mahindi

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

BAADHI ya wakulima wanaoishi vijiji vya mipakani mkoani Rukwa wameiomba serikali kudhibiti njia za panya zinazoingia na kutoka nchini, ili kudhibiti watu wa nchi jirani kutumia mwanya huo kuingiza mahindi na kuyauza kwa Wakala wa Chakula wa Taifa (NFRA).

Ombi hilo walilitoa jana wakizungumza na mwandishi wa habari hizi kwa nia ya kuishukuru serikali kwa uamuzi wa kutoa Sh. bilioni 50 ili zitumike kununua mahindi kwa wakulima ambao walikuwa hawana pa kuyauza kwa kukosa soko.

Mmoja wa wakulima hao, Calvin Mapesa, mkazi wa Kijiji cha Kipwa, Wilaya ya Kalambo aliiomba serikali kudhibiti njia za panya ili kuhakikisha raia kutoka nchi za jirani wasije kuingiza mahindi nchini na kuyauza NFRA hatua itakayosababisha baadhi ya wakulima kushindwa kuuza mahindi yao.

Alisema miaka ya nyuma wakati serikali inatoa pembejeo za kilimo, baadhi ya raia wa kigeni walikuwa wakiingia nchini kwa njia za panya na kununua pembejeo hizo kwa wakulima wanaopata pembejeo za ruzuku.

"Tuna uzoefu katika hili, miaka ya nyuma Wazambia walikuwa wanaingia kinyemela humu nchini na kuja kuwalaghai wakulima waliokuwa wanapata mbolea za ruzuku na kununua kwa wakulima hao na kisha kwenda kutumia nchini kwao, pia wanaweza kuingia na mahindi yao wakashirikiana na Watanzania wasio wazalendo na wakafanikiwa kuuza mahindi yao NFRA, tunaomba serikali iwe makini," alisema.

Naye Joyce Sikavizya, mkazi wa Kijiji cha Mtowisa wilayani Sumbawanga alimshukuru Rais Samia Hassan kwa uamuzi mgumu wa kuamua kununua mahindi ya wakulima kitendo kitakacho wapa morari wakulima ili katika msimu ujao wa kilimo wajitume kuzalisha zaidi mazao mbalimbali kwa kuwa watakuwa na fedha za kununulia pembejeo.

Alisema hivi sasa mkulima atapata ahueni ya maisha kutokana wengi walikuwa wanakabiliwa na hali ngumu ya maisha ikiwamo kushindwa kuzihudumia familia zao kwa kukosa fedha kutokana na kukosa soko zuri la mahindi.

# Mkakati waja kuwapa wengi chanjo corona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imekuja na mkakati wa kuhamasisha wananchi wengi kujitokeza na kupata chanjo ya corona.

Katika kutekeleza mkakati huo, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, amesema kuwa serikali imepanga kufanya wiki ya uchanjaji wa chanjo ya UVIKO-19 nchi nzima ili kupeleka huduma hiyo karibu na wananchi.

Msigwa, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akitoa taarifa yake kwa waandishi wa habari.

"Serikali vitu ambavyo inaviangalia sasa ni kuhakikisha kuwa tunakuwa na wiki ya uchanjaji, utaratibu huu sasa unaandaliwa au unakamilishwa na mwishoni mwa Septemba au Oktoba mwaka huu mwanzoni tutakuwa na wiki ya uchanjaji chanjo ya UVIKO-19 katika maeneo mablimbali nchini," alisema Msigwa.

Kadhalika, alisema katika wiki hiyo ya uchanjaji, viongozi wa nchi nzima watashiriki moja kwa moja kwenye wiki hiyo kuhakikisha Watanzania wengi wanapata chanjo ili kuepukana na madhara ya ugonjwa huo.

"Zaidi ya Watanzania 345,000 wameshapata chanjo ya UVIKO- 19 hadi kufikia leo (jana) katika zile chanjo tulizoletwa nchini na matarajio yetu tuendelee mbele zaidi, lakini serikali inaendelea kuangalia namna nyingine ya kuleta chanjo nyingine ili Watanzania waendelee kupata chanjo," alisema Msigwa.

Hata hivyo, Msigwa, alitoa wito kwa Watanzania ambao hawajapata chanjo hiyo kujitokeza kwa wingi katika wiki ya uchanjaji.

"Natoa wito kwa Watanzania kujitokeza kuchanja kwa wingi katiki wiki hiyo hasa wale ambao wapo katika mazingira hatarishi kwenye jamii yetu," alisisitiza Msigwa.

Aidha, Msigwa alisema hadi sasa nchi imefikia asilimia 34, ya utoaji wa chanjo hiyo na kutoa wito kwa wananchi kuendelea kujitokeza kwa wingi kupata chanjo hiyo ya UVIKO-19 inayotolewa bure na serikali.

Pia, alisema baada ya majadiliano ya muda mrefu na Shirika la Fedha Duniani (IMF), sasa limeidhinisha maombi ya Sh. trilioni 1.3 kwa ajili ya kusaidia maeneo mbalimbali yalioathiriwa na UVIKO-19.

Alifafanua kuwa kiasi hicho cha fedha kitakwenda kutumika katika kuboresha miundombinu ya elimu, utalii na maji.

"Mnafahamu Dunia ikiwamo Tanzania imepata madhara ya UVIKO-19... maeneo ya uzalishaji yameathirika, maeneo ya utalii yameathirika, maeneo ya huduma za kijamii yameathirika kwa hivyo serikali iliamua kuomba fedha hizo kiasi cha Dola milioni 567.25 baada ya majadiliano ya muda mrefu, fedha hizo sasa zimeidhinishwa na bodi ya wakurugenzi na zipo tayari kuanza kuletwa nchini," alisema Msigwa.

Alisema, kupitia fedha hizo wanategemea kujenga vyumba vingi vya madarasa ili wanafunzi wasikae chini, kutengeneza madawati na kuwa na miundombinu mizuri ya elimu.

Vilevile, alisema fedha hizo zinakwenda kuboresha miundombinu ya utalii pamoja na ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha chanjo kinachokadiriwa kutumia Sh. bilioni 83.

"Hiki kiwanda siyo kwa ajili ya chanjo ya UVIKO-19 pekee bali ni kwa ajili ya kuzalisha chanjo za magonjwa mbalimbali ya binadamu," alisema Msigwa.



Mkurugenzi wa ITCoEICT wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Dk. Greyson Alila (kushoto), akitoa maelezo kwa wageni waliotembelea taasisi hiyo kufuatilia maendeleo ya mradi wa kituo cha umahiri cha TEHAMA (ITCoEICT), kilichoanzishwa kwa ushirikiano wa Serikali ya India na Tanzania. Kulia ni Mkuu wa Taasisi hiyo, Prof. Preksedis Ndomba, (wa pili kulia) Balozi wa India nchini Tanzania, Binaya Pradhan, ziara iliyofanyika mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Vituo vya mafuta vilivyojengwa holela kupewa masharti magumu

**Na Joseph Mwendapole**

VITUO vya mafuta vilivyojengwa chini ya umbali wa mita 200 kama sheria inavyotaka vitawekewa masharti magumu ili viweze kuendelea na biashara hiyo.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, wakati akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki.

Alikuwa akizungumzia operesheni inayoendelea nchi nzima ya kubaini vituo vinavyoendeshwa bila kuwa na vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) na kuvitoza faini.

Dk. Gwamaka alisema mbali na adhabu kwa kujenga kinyume na taratibu, vituo hivyo vitalazimika kutimiza masharti magumu kama ya kuweka mifumo madhubuti ya kukabiliana na majanga endapo yatatokea.

"Vituo vilivyojengwa chini ya umbali wa mita 200 havitabomolewa badala yake vitawekewa masharti magumu kama kuweka mifumo ya gharama kubwa kuhakikisha iwapo litatokea janga basi mifumo hiyo inadhibiti kwa haraka," alisema.

"Sasa gharama za uendeshaji wa vituo hivi lazima itakuwa kubwa kulinganisha na vile ambavyo vimejengwa kwa kufuata sheria kwasababu huyu aliyejenga kiholela kuna mambo atatakiwa kuyafanya ambayo yatamgharimu fedha nyingi," alisema.

Wiki iliyopita NEMC ilivitoza faini ya jumla ya Sh. bilioni 5.1 kampuni tisa za mafuta zilizojenga vituo vya mafuta bila kuwa na vyeti vya EIA.

NEMC ilisema vituo vyote hivyo vinapaswa kuhakikisha vinalipa faini hiyo ndani ya siku 14 kuanzia Ijumaa iliyopita na kutaka wengine wanaojijua kwamba hawana vyeti hivyo kujisalimisha wenyewe kwenye Baraza kabla hawajafikiwa waliko. Dk. Gwamaka alisema kwenye msako unaoendelea kwenye mikoa yote nchini wamegundua vituo 393 vya mafuta ambavyo havina vyeti vya EIA, lakini vinaendelea na shughuli zake kama kawaida.

Alizitaja kampuni hizo kuwa ni Oryx yenye vituo 15 ambavyo havina vyeti vya EIA na kampuni imetozwa faini ya Sh. milioni 750.

Alitaja kampuni nyingine kuwa ni PUMA yenye vituo 22 vyote jumla vimetozwa faini ya Sh. bilioni 1.1, kampuni nyingine ikiwa Total yenye vituo 16 ambayo imetozwa faini ya Sh. milioni 800.

Dk. Gwamaka alitaja kampuni nyingine kuwa ni Camel Oil yenye vituo sita ambavyo imetozwa faini ya Sh. milioni 300, GBP yenye vituo 10 iliyotozwa Sh. milioni 50 na GAPCO yenye vituo nane iliyotozwa faini ya Sh. milioni 400.

Alitaja kampuni zingine kuwa ni Ester Oil yenye vituo tisa ambayo imetozwa faini ya Sh. milioni 450, Oil Com vituo 12 imetozwa faini ya Sh. milioni 600 na TSN yenye vituo vinne imetozwa faini ya Sh. milioni 200.

"Hawa niliowataja ni baadhi tu kwasababu msako bado unaendelea nchi nzima na tutaendelea kuwatangaza na faini wanazopewa kila tunapowabaini maana mbali na kukosa vyeti vya EIA wanaikosesha serikali kodi ambayo wangepeswa kuilipa," alisema.

Wiki iliyopita pia (NEMC), iliitoza ya Sh. bilioni 3.3 Kampuni ya Mafuta ya Lake Oil inayotuhumiwa kujenga vituo vingi vya mafuta maeneo mbalimbali nchini bila kuwa na vyeti vya EIA.

## HABARI KITAIFA

# Kauli ya Ndugai safari za mawaziri Dar yaibua wadau

**Na Waandishi Wetu**

KITENDO cha baadhi ya mawaziri na watendaji wa serikali kuendelea kung'ang'ania jijini Dar es Salaam wakifanya mikutano, semina na makongamano badala ya mkoani Dodoma, kimewaibua wasomi na wachambuzi ambao wamesema hali hiyo itaendelea kudidimiza uchumi wa nchi na maendeleo.

Wamesema hatua hiyo itaendeelea kuongeza mzigo wa gharama kwa serikali hususani wananchi.

Hoja ya baadhi ya viongozi wa serikali kutokukaa Dodoma badala yake wakikimbilia jijini Dar es Salaam kufanya makongamano na semina mara kwa mara ilielezwa mwishoni mwa wiki bungeni na Spika Job Ndugai.

Spika Ndugai alieleza kuwa magari ya viongozi wa serikali yamekuwa 'yakitiririka' kila wakati kuelekea jijini Dar es Salaam kutokea Dodoma, baada ya siku mbili yanarudi Dodoma.

Alisema hali hiyo inaongeza gharama za matumizi kwa serikali kwa sababu kiongozi akielekea jijini Dar es Salaam kutoka Dodoma kuna gharama za malipo kwa wasaidizi wake, dereva na yeye mwenyewe (kiongozi).

Spika Ndugai alisema: "Hatusemi Dar es Salaam kusifanyike chochote, kuna wakati Waziri Mkuu nilimuuliza nani anaidhinisha Government Expenditure (gharama za matumizi za serikali)." Akizungumza na Nipashe, Mbunge wa Viti Maalum, Kunti Majala, alisema Spika Ndugai yupo sahihi kuhoji uwapo wa hali hiyo kwa kuwa wizara zote zipo Dodoma na hakuna sababu za msingi kufanyia semina, vikao na makongamano jijini Dar es Salaam.

"Sababu gani za msingi zinazosababisha kiongozi atoke hapa (Dodoma) aende Dar es Salaam akalipwe posho za kulala mafuta, hata vipuli vya magari vinachakaa kwa sababu Dodoma kuna ofisi na ni eneo lake la kazi, sasa kwanini wawe na maamuzi mengine tofauti, Spika yupo sahihi tunaamini serikali imesikia na itaenda kufanyia kazi," alisema Majala.

Mbunge wa Bukene (CCM), Selemani Zedi, alisema: "Nakubaliana na kauli ya Spika kwa sababu jitihada zozote za kupunguza gharama zinastahili kuungwa mkono ni muhimu serikali kuzingatia kauli ya Spika."

Mkuu wa Idara ya Uenezi na Mawasiliano ya Umma wa Chama cha NCCR-Mageuzi, Edward Simbeye, alisema tatizo kubwa linalochangia shughuli nyingi za serikali kufanyika Dar es Salaam ni kutokana na kukosekana kwa miundombinu ya kuwezesha kufanyika kwa shughuli hizo jijini Dodoma.

"Ni kweli makao makuu ya nchi ni Dodoma, lakini bado hakuna miundombinu ya kuwezesha shughuli zote kufanyika katika jiji hilo, tumefanya haraka kuhamisha serikali wakati bado hatujajipanga, " alisema na kuendelea:

"Shughuli nyingi zinafanyikia Dar es Salaam kwa sababu ndiyo mji ambao unamiundombuni ya kuwezesha hizo shughuli."

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Grace Tendega, alisema viongozi wa serikali kukimbilia Dar es Salaam hali hiyo itazidi kuongeza gharama ya matumizi kwa serikali.

Alisema: "Kwenda Dar es Salaam ni sawa, lakini kuwe na kitu maalum ambacho hakiwezi kufanyika Dodoma, kama vile mkutano wa kuchukua watu wengi zaidi."

Mchambuzi wa masuala ya kisiasa, Gwandumi Mwakatobe, alisema hatua ya viongozi wa umma ikiwamo mawaziri kuendelea kufanyia shughuli zao jijini Dar es Salaam, kunaongeza mzigo kwa serikali hasa mwananchi. Alisema serikali ilishaamua kuhamishia shughuli zake pamoja na ofisi jijini Dodoma kunaongeza gharama kwa serikali, kwamba fedha hizo zingetumika katika sekta za maendeleo znazomgusa mwananchi moja kwa moja.

Gwandumi alisema wakati Spika Ndugai akitoa kauli hiyo ni wakati mwafaka kwa Bunge lianze kwa kujitathmini lenyewe kwanza kwa kuwa wabunge ndiyo wanaongoza kuwa nje ya majimbo yao.

Alisema: "Bajeti nyingi kwa nchi za Afrika zinatumika katika matumizi ya kawaida kwa zaidi ya asilimia 70, matumizi hayo ni kwa ajili ya shughuli za ofisi, posho za vikao, chai, badala ya fedha kutumika katika shughuli za maendeleo."

**Imeandaliwa na Augusta Njoji (Dodoma), Elizaberth Zaya na Christina Mwakangale (Dar)**


### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Pili Mkaka Makunenge** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba **T881 DLX** akiwa eneo la Rukaragata Wilayani Biharamulo.Taarifa za kupotea kwa kadi zimetolewa katika kituo cha Polisi na kufunguliwa jalada namba **KAG/BIH/RB/436080/202** Atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

### PASSPORT IMEPOTEA



**LILIANE BRUNO KAHANGWA** anatangaza kupotelewa kwa hati yake ya kusafiria (passport) yenye namba za usajili **AB185433.** Kwa yeyote atakae kiona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Rb Namba. **MOR/MOR/RB/443184/2021**

116454402

**JUDICIARY SUMMONS TO DEPENDANT**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI;MDAIWA**
**[MCA/63]**
**MAHAKAMA YA MWANZO YA MWANJELWA WILAYA YA MBEYA**
**SHAURI YA MADAI YA MIRATHI....................121................2012**

MDAI ;MSIMAMIZI ........FRANKLIN ROBERT NKUBA
MDAIWA;MAREHEMU........ROBERT MWANDU NKUBA
KWA;SAMSON ROBERT MWANDU WA DAR ES SALAAM
KWA KUWA MDAI /WADAIWA AMELETA /WAMELETA MADAI YAKO/YAO KWAMBA [ELEZA HAPA HABARI ZA MADAI KWA KIFUPI] NI JUU YA MIRATHI YA MAREHEMU ROBERT MWANDU NKUBA ....................KWA HIYO UNAHITAJIWA/ANASHITAKIWA KUHUDHURIA BINAFSI KATIKA MAHAMA HII SIKU YA JUMATANO 1/9/2021 SAA 230 ASUBUHI /ALASIRI KWA KUJIBU MADAI HAYA NA KWA KUWA SIKU HIYO NI SIKU YA KUKATWA SHAURI HILO NI LAZIMA KULETA MASHAHID WAKO/WENU NA HATI ZOTE ZINAZOHUSU SHAURI HILO KWA AJILI YA KUJITETEA KATIKA SHAURI HILO. ANGALIA KAMA HUKUHUDHURIA SIKU HIYO ILIYOTAJWA HAPO JUU MAHAKAMA IKITHIBITISHA KAMA UMEPOKEA KUITWA SHAURINI ITAWEZA KUTOA HUKUMU UMESHINDWA/AMESHINDWA.HATI HII INATOLEWA KWA AMRI YANGU NA CHAPA YA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 26...8.....2021.

..........................................................................

HAKIMU WA MAHAKAMA YA MWANZO
FAHAMU;
1]IWAPO UNAFIKIRIA KUWA MASHAHIDI WAKO/WENU HAWATAHUDHURIA KWA HIYARI YAO WENYEWE UNAWEZA/MNAWEZA KUPEWA KUITWA SHAURINI KATIKA MAHAKAMA HII YA KUWA LAZIMISHA MASHAHIDI WOTE WAHUDHURIE NA KUPELEKA HATI YOYOTE AMBAYO INAHITAJIWAMBELE YA MAHAKAMA,UNAWEZA /UNAWEZA/UNAWEZA KUIOMBA MAHAKAMA KWA KULIPA ADA IPASAVYO.
2]IWAPO UNAKUBALI /MNAKUBALI DENI HILO,KUEPUKA NA KUTIMILIZWAKWA MAHAKAMA HUENDA AKAWA JUU YAKO/YENU AU MALI YAKO/YENU AU YOTE WAWILI.
NIMEPOKEA NAKALA YA KUITWA SHAURINI HII LEO TAR.................................
SAHIHI YA MWENYE KUPELEKEWAHATI HII............................
SAHIHI YA MWASILISHAJI.......................
TAREHE...........................

TRA

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

### WAHARIBIFU WA MINADA KWA NJIA YA MTANDAO

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mara kwa mara inaendesha minada kwa njia ya mtandao yaani **Online Auctions** kwa mizigo iliyoshindwa kukamilisha taratibu za forodha na kupitisha muda kwa mujibu wa sheria ya Forodha ya Jumuia ya Afrika Mashariki. Katika ushiriki wa minada hii, Mamlaka ya Mapato inapenda kuutaarifu umma kwamba, wapo washiriki wa minada ambao wanashinda na kuacha kulipia bidhaa husika kwa mujibu wa vigezo na masharti vilivyowekwa katika uendeshaji wa minada hivyo wametenda kosa la kuharibu mnada kwa makusudi.

Hivyo, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatoa wito kwa washiriki hao kuacha kitendo hicho maramoja kwani ni kosa kisheria, na hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakaebainika kujihusisha au kwenda kinyume na masharti na taratibu za mnada kama sheria inavyoelekeza

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na:
**KAMISHNA WA FORODHA NA USHURU WA BIDHAA**

216454802

# Majaliwa atia neno ujenzi wa SGR

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekagua mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha Dar es Salaam hadi Kilosa, mkoani Morogoro na kusema ameridhishwa na hatua iliyofikiwa.

"Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria kukamilisha ujenzi wa miradi yote iliyoanzishwa, hivyo Watanzania waendelee kuwa na imani na serikali yao, na tunawahakikishia mradi huu utakamilika kwa wakati."

Waziri Mkuu alitoa kauli hiyo jana wakati akikagua maendeleo ya ujenzi ya mradi huo katika kituo cha Kwala kilichoko mkoani Pwani, ambacho kitatumika kama kituo kikuu cha kufanya matengenezo makubwa ya mabehewa na injini za treni.

"Maendeleo ya ujenzi huu yanatia matumaini na kazi inaendelea kwa ufanisi na eneo lililobaki la Pugu Dar es Salaam tunaamini litakamilika kwa wakati, nimeridhishwa na vituo vya abiria vilivyokamilika."

Aidha, Waziri Mkuu aliwasihi wafanyakazi wa mradi huo kufanya kazi kwa ufanisi kwani lengo la serikali ni kuufikisha mradi huo katika mikoa ya Mwanza, Kigoma, Katavi katika Bandari ya Karema.

"Njia zote za reli tunataka ziwe za kisasa, hii pia itawezesha kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, nchi yetu ni ya kimkakati kwa sababu nchi zote za jirani zinategemea reli hii," alisema.

Aliongeza kuwa kukamilika kwa mradi huo kutaongeza ufanisi wa usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kupunguza muda wa safari, kutoka Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma na Mwanza.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Massanja Kadogosa, alisema hadi kufikia Agosti mwaka huu, ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro ulikuwa umefikia asilimia 93.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo alisema kuwa ujenzi wa kipande cha pili cha mradi huo kinachoanzia Morogoro hadi Makutopola (Singida) ulikuwa umefikia asilimia 70.11.

Alisema SGR ikikamilika itachochea mipango ya serikali ya awamu ya sita katika kutekeleza sera ya viwanda na kuifikisha Tanzania kwenye uchumi wa kati wa juu ifikapo mwaka 2025.



Mawakala wa utalii kutoka nchini Georgia wakiwasili Uwanja wa Ndege wa Arusha kutembelea vivutio vya utalii vilivyoko mashariki mwa Tanzania, ikiwa ni hatua za awali za kukamilisha mchakato wa kuanza kuleta makundi ya watalii kutoka nchi hiyo. **PICHA: ASRAJI ASIRAJI MVUNGI**

# W'biashara 9 wakutwa na kesi ya kujibu dhidi dawa za kulevya

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imesema wafanyabiashara tisa akiwamo nguli wa biashara za dawa za kulevya, Mwanaidi Ramadhani, wana kesi ya kujibu dhidi ya kuingiza dawa hizo aina ya cocaine, kilo tano.

Mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Isaya Arufani, ilitoa uamuzi huo baada ya upande wa Jamhuri kudai kuwa umefunga kesi yake dhidi ya washtakiwa.

Kabla ya kufunga kesi hiyo upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Monica Mboga, ulimwongoza shahidi wa mwisho, Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Mbezi A, John Masinga. Masinga alidai kuwa mwaka Juni Mosi, 2011 saa sita kasoro usiku alikuwa nyumbani kwake, alipigiwa simu na mjumbe wa shina Swati Kibona (kwa sasa marehemu).

Alidai kuwa Kibona alimweleza kwamba kuna watu wa usalama wamefika mtaani wako wanahitaji ushirikiano wao eneo la Mwanamboka.

"Nilikwenda Mtaa wa Almas kukutana na Kibona na watu wa usalama ili twende eneo la tukio, nilimkuta akiwa na askari," alidai na kuongeza.

"Tulikwenda kwenye nyumba mtaani hapo, tulikuta watu wako chini ya ulinzi, askari kiongozi wa upekuzi alitueleza lazima wajumbe tushuhudie wakati upekuzi unafanyika," alidai shahidi.

Aidha, alidai kuwa askari walimwamuru mama mwenye nyumba Mwanaidi Ramadhani kuwaongoza kwenda chumbani kwake.

"Tulivyofika chumbani kwake askari mwanamke alianza kupekua chini ya godoro la kitanda chake tulikuta pakiti mbili zikiwa zimeandikwa coffee, askari alitueleza ni dawa za kulevya, tulipata fedha za mataifa mbalimbali zikiwamo za kitanzania na hati za kusafiria mtuhumiwa alirudishwa tulipomtoa," alidai Masinga.

Akifafanua ushahidi wake, alidai kuwa alichukuliwa mshtakiwa wa pili Sara Daudi, akawaongoza chumbani kwake baada ya upekuzi walipata pakiti moja ya kaki ikiwa na dawa za kulevya, chooni juu ya tangi la maji askari alikuta kifurushi kimefungwa dawa hizo pia. Mbali na vyumba hivyo, shahidi alidai kuwa walikwenda chumba kilichokuwa kinatumika na wageni wawili wanaume wa Mwanaidi, baada ya upekuzi kwenye begi kubwa ndani yake walikuta bahasha mbili zenye unga wa kahawa, fedha na chooni walitoa kifurushi kingine.

Shahidi huyo wa mwisho wa Jamhuri alidai kuwa askari waliorodhesha kila walichokamata ndani ya nyumba hiyo mbele yao, wakatia saini.

Mbali na Mwanaidi na Sara, washtakiwa wengine ni, Anthony Karanja, Ben Ngare, Almas Said, Yahaya Ibrahim, Aisha Kungwi na Rajabu Mzombe, ambao walisomewa mashtaka yao kwa mara ya kwanza 2011 mpaka sasa ni miaka 10, wako mahabusu.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa, Juni Mosi, 2011, eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, washtakiwa walikamatwa wakiingiza dawa za kulevya aina ya cocaine.

Washtakiwa walikana mashtaka hayo.

# Samia kuzindua mkakati wa sensa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, kesho anatarajiwa kuzindua Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti mwaka 2022.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, alieleza hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo.

"Ndugu waandishi wa habari nimewaita hapa leo ili kuwajulisha kuwa mkoa wetu umepewa heshima ya kuwa mwenyeji wa tukio hilo kubwa la kitaifa la uzinduzi wa kitabu cha mkakati wa uelimishaji na uhamasishaji wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022," alisema Mtaka.

Alisema, mkakati wa uelimishaji na uhamasishaji una lengo la kuuandaa umma na wadau wote kwa ujumla ili kila mmoja kwa nafasi yake aweze na awezeshe kufanikiwa kwa zoezi hilo kwa ufanisi unaotarajiwa ifikapo mwaka 2022.

"Uzinduzi wa mkakati huo utafanyika Septemba 14, mwaka huu katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, ambapo mgeni rasmi ni Rais Samia Suluhu Hassan," alisisitiza Mtaka. Alisema, pamoja na Rais tukio hilo, pia litahudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati Kuu ya Taifa ya Sensa, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla, ambaye ni Mwenyekiti mweza wa Kamati ya Taifa ya Sensa.

Alisema viongozi wengine ni Kamisaa wa Sensa Tanzania Bara, Spika mstaafu Anne Mkinda, Kamisaa wa Sensa Zanzibar, Balozi Mohamed Haji Hamza, pamoja na mawaziri na manaibu, makatibu wakuu na manaibu pamoja na wadau wa maendeleo.

"Kama mnavyofahamu, serikali imepanga kufanya sensa ya watu na makazi mwezi Agosti 2022 katika siku itakayotangazwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema Mtaka.

Alisema madhumuni makubwa ya kufanya senza ya watu na makazi ni kupata takwimu za msingi za watu na hali ya makazi ambazo zitasaidia kutunga sera na kupanga mipango ya maendeleo ya kimkakati inayolenga kukuza usatawi wa nchi na watu wake. "Takwimu hizo pia hutumika kupima kiwango cha maendeleo kilichofikiwa pamoja na kuandaa miongozo itakayotumika katika kutayarisha mipango ya maendeleo ya muda mfupi na muda mrefu," alisisitiza Mtaka.

HABARI KITAIFA

# Mbunge ataka Tanzania iwe na Sheria ya Usalama wa Chakula

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum kupitia kundi la asasi za kiraia (NGO), Neema Lugangira, amesema Tanzania inahitaji Sheria ya Usalama wa Chakula na suala hilo kusimamiwa chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki akichangia Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Viwango vya Afya ya Mimea, Afya ya Wanyama na Usalama wa Chakula.

Alisema ni vema suala la usalama wa chakula kuwa chini ya wizara hiyo na kuwa kama Taifa ili kukidhi matakwa ya itifaki hiyo inahitajika Sheria ya Usalama wa Chakula.

"Ningependa kuishauri serikali kwenye eneo zima la usalama wa chakula kwa suala hilo kuratibiwa chini ya Wizara ya Afya kwa sababu maana ya usalama wa chakula ni kuona namna gani ambavyo utalinda walaji wasipate changamoto zozote zinazotokana na chakula," alisema.

"Jambo hili ni jukumu la Wizara ya Afya, hapa kwetu tumeweka jukumu la usalama wa chakula chini ya TBS... napenda kuishauri serikali maadam tumeridhia azimio hili, lazima tutafakari upya na tufanye mabadiliko," alisema na kuongeza:

"Naipongeza Wizara ya Kilimo kwa sababu wameimarisha usimamizi kwenye afya ya mimea chini ya TPRI, kwani moja ya matakwa ya itifaki hii duniani ni lazima nchi iwe na sheria ya usalama wa chakula."

Alisema Tanzania hatujawa na sheria ya usalama wa chakula, hivyo alisisitiza kuwa kwa kuwa wabunge wamelikubali azimio hilio, serikali ifanye jitihada za haraka kutuletea sheria ya usalama wa chakula ili nchi iendane na takwa hili la kidunia.

Neema alisema ndani ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ni Kenya peke yake ambayo imeshakuwa na sheria ya usalama wa chakula na kuwa kwa mantiki hiyo Tanzania kuendelea kutokuwa na sheria hiyo, kuna maeneo ambayo haitanufaika ipasavyo.

"Naomba nishauri serikali ni namna gani baada ya azimio hili itakuwa limeridhiwa basi usimamuzi wa masuala ya afya ya mazao ya kilimo yatakuwa chini ya Wizara ya Kilimo," aliongeza.

Mbunge huyo alisema ni muhimu wakulima na wananchi kwa ujumla kupewa elimu ya itifaki hiyo ili waweze kukidhi vigezo vyake na kunufaika nayo.



Ofisa Msimamizi Mwandamizi wa Kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Mara, Zake Wilbard, akifafanua jambo wakati wa semina ya mabadiliko ya sheria za kodi ya mwaka 2021 iliyofanyika mjini Bariadi mkoani Simiyu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chanika, Majohe na Msongola kupata neema ya umeme

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Umeme Nchini (TANESCO) Ilala limewataka wakazi wa Chanika, Majohe na Msongola kuondoa wasiwasi kuhusu kero ya kuunganishiwa umeme majumbani.

Akizungumza na wananchi wa maeneo hayo katika ziara mwishoni mwa wiki, Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja wa Ilala, Deusdedit Hokororo, alisema amepokea malalamiko yao na wanayafanyia kazi ili wananchi hao kuvutiwa umeme.

Awali, wananchi walielezea masikitiko ya kuchelewa kwa ukaguzi na upatikanaji wa nguzo na vitendo vya rushwa kwa viongozi wao wa mitaa jambo ambalo linawakwamisha kupata huduma hizo kwa wakati.

Mkazi wa Msongola, Asteria Majihuka, alisema wamepata faraja kwa watendaji wa shirika kuwatembelea na kusikia huku wakiwaahidi kuwatatulia.

Alidai baadhi ya kero hizo ni pamoja na nguzo kutowafikia na zikifika mtaani kuna vitendo vya hujuma na rushwa.

"Nilishakata tamaa kabisa nimefuatilia mpaka nikaamua kuuza mafriji yangu na baadhi ya vitu vinavyotumia umeme kwa kuwa sikua na matarajio tena, lakini kwa sasa tunashukuru tumepata mwangaza," alisema.

Diwani wa Viti Maalum Msongola, Magdalena Thomas, alisema wananchi walikua wakimlalamikia usumbufu wa nguzo zinafikishwa 100 zinakidhi mitaa mitatu au minne na kuisha bila kuwafikia wananchi wengi wenye mahitaji.

Alisema TANESCO imewaahidi, anaamini tatizo litaisha kwa wananchi hao.

Akitoa mfano katika hilo, Hokororo alisema awali Ilala ilikuwa na wakaguzi wachache, lakini sasa wameongezeka na wamepelekwa mitaani kufanya kazi usiku na mchana.

Aliwaasa pia kutotumia vishoka waliozagaa mitaani kwa kuwa huduma hizo za umeme wanafungiwa kwa bei nafuu.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **AVATOR TANZANIA LIMITED, MAGNUM AND SONS AUCTION CO LTD, JOSINA COMPANY LIMITED AND AUCTIONEER na MAK RECOVERIES LTD** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD,** Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| NOTISI KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA | | | |
|---|---|---|---|
| AVATOR TANZANIA LIMITED | | | |
| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 1 | FLORA RAPHAEL MWANDUPE | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Salasala, Kinondoni – Dar Es Salaam |
| 2 | HAJI A SILAYO | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Sagale,Viziwaziwa - Kibaha Pwani |
| 3 | HAWA SAID | Vitu Vya Nyumbani na Biashara | Msasani, Kinondoni - Dar Es-Salaam |
| 4 | MARIA ABEL MAYA | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Nyakasangwe, Wazo hilli - Dar Es Salaam |
| 5 | SHABANI S MAGANGA | Nyumba Yenye Mkataba Wa Mauziano | Kilimahewa, Tangini - Kibaha |
| 6 | JUSTINA JOSEPH MREMA | Kiwanja Chenye Mkataba Wa Mauziano | Nyakasangwe, Wazo Hill - Dar es Salaam |
| JOSINA COMPANY LIMITED AND AUCTIONEER | | | |
| 7 | MAXIMILIAN K. KATO | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | KIBETA - BUKOBA |
| 8 | LAURENT M. THADEO | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | IROGELO KAMACHUMU - BUKOBA |
| 9 | NISEPH PAPIUS THEODORY | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | RWAMISHENYE KAGONDO KAIFO- BUKOBA |
| 10 | JASSON BISHAIJA | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | BULILA- BUKOBA |
| 11 | JEVINA G. GWAGUBELITI | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | BUSHAGA NSHAMBYA - BUKOBA |
| 12 | ALFRED R. BENARD | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | KASHAI KISIND I- BUKOBA |
| 13 | HONORATH R. BAYONA | Nyumba yenye mkataba wa mauziano na kiwanja chenye mkataba wa mauziano | KAGONDO KAIFO - BUKOBA |
| 14 | SHAMIMU K. ELIA | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | BUSHAGA NSHAMBYA - BUKOBA |
| MAGNUM AND SONS AUCTION MART CO LTD | | | |
| 15 | MONICA S. ASENGA | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Ambureni (Barabara Mpya) - Arusha |
| 16 | LOISHIYE E. MOLLEL | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Kisongo - Arusha |
| 17 | STEPHEN G. MASSAWE | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Ngaramtoni - Arusha |
| 18 | ROBERT L MKENDYA | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Kisongo - Arusha |
| 19 | JACKSON N KOMBE | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Engo Sengiu - Arusha |
| MAK RECOERIES LIMITED | | | |
| 20 | MAGRETH PATRICK MALINGA | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Kiranyi - Arusha |
| 21 | LUKA B NG'OJA | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Muriet - Arusha |
| 22 | FATUMA M MJEMA | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Engo Sengiu - Arusha |
| 23 | PRINCIPAL PETER MBOYA | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Muriet - Arusha |
| 24 | FRANK SIMBO KOMBE | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Moshono - Arusha |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipa ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada, Kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (Transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA SIMU NAMBA**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Magnum and son Auction Co Ltd.**
**P.O. Box 1763 Arusha**
**Namba 0757151530/0768247735**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Mack Recoveries Ltd**
**P. O. Box 2052 Dar es salaam**
**0715 375475/ 0783224965**

**0716 35 3650/0763 481 798**

**Mkurugenzi mtendaji,**
**Avator Tanzania Limited**
**P. O. Box 18082 Dar es salaam**
**Mobile: 0715800016/ 0682587760**

**Mkurugenzi Mtendaji.**
**Josina Company Limited and**
**Auctioneer**
**P. O. Box 11126, Mwanza**
**Mobile: 0713 203040**

**Na**
**Finca Microfinance Bank Ltd**
**P. O. Box 78783, Dar es Salaam**
**Mobile: 0768790399, 0754774949**

216454902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wawakilishi wetu michuano CAF msilale bado dakika 90

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa walioanzia hatua ya awali, Yanga, Azam FC na Biashara United, tayari wamemaliza dakika 90 za kwanza na kilichobaki ni muda mwingine kama huo zitakaporudiana mwishoni mwa wiki hii.

Katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), Yanga na Simba zinaiwakilisha Tanzania Bara kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini 'Wekundu wa Msimbazi' hao wao wanaanzia moja kwa moja kwenye raundi ya kwanza.

Kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika, Azam FC na Biashara United ndizo zinazobeba jukumu hilo la kuhakikisha bendera ya Tanzania inapepea vema kimataifa katika michuano hiyo ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu Afrika baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa.

Ukiacha matokeo ya jana kati ya Yanga na Rivers United ya Nigeria ambayo hadi gazeti hili linakwenda mitambo timu hizo zilikuwa bado hazijafungana kwenye mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, upande wa pili Azam FC na Biashara United zimeanza vema kinyang'anyiro hicho.

Biashara United ambayo ilianzia ugenini dhidi ya Dikhil ya Djibouti, iliibuka na ushindi wa bao 1-0 wakati Azam FC nayo ilipata ushindi mnono nyumbani katika Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam baada ya kuichapa Horseed ya Somalia mabao 3-1.

Kwa ujumla ni matokeo mazuri kwa wawakilishi wetu hao, lakini hawapaswi kubweteka na kusahau kujipanga vema kuelekea mechi za marudiano mwishoni mwa jumla kwa kuwa hizo ni dakika 90 za kwanza bado zingine kama hizo na lolote linaweza kutokea kwenye mechi za marudiano kwa wapinzani wao kupindua meza.

Kwa Yanga yenyewe itakuwa ugenini nchini Nigeria, hivyo inapaswa kufanya maandalizi makubwa zaidi na kujipanga kwa kila kitu ndani na nje ya uwanja hususan kuwaandaa wachezaji kisaikolojia kwa kila kitakachotokea.

Lakini kwa Azam FC kama ilivyo kwa Biashara United, zenyewe zitakuwa nyumbani katika mechi hizo za marudiano, lakini hilo haliwezi kuwa sababu ya kuacha kujiandaa vema kwani mara nyingine mpira una matokeo ya ajabu na wapinzani wao wanaweza kupata matokeo chanya na kuwatoa.

Tunaamini kama Biashara United ilishinda ugenini, pia Dikhil inaweza kujipanga na kupata ushindi kwenye mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, hivyo kikubwa wawakilishi hao wa Tanzania wote kwa ujumla hawapaswi kuwadharau wapinzani wao na badala yake wanatakiwa kufanya maandalizi makubwa zaidi.

Kwa Azam FC ambayo imepata bahati ya mechi zote mbili kuchezwa hapa nchini kutokana na hali ya usalama Somalia kutokuwa shwari, bado hawapaswi kubweteka na kusahau kujipanga vizuri kwani lolote linaweza kutokea na Wasomali hao kupata matokeo chanya yatakaowawezesha kusonga mbele.

Aidha, pamoja na mashabiki kutoruhusiwa kuhudhuria mechi hizo kutokana na janga la ugonjwa wa COVID-19 linaloitesa dunia, wachezaji na makocha hawana budi kutambua wadau wa soka nchini na Watanzania kwa ujumla wapo nyuma yao kwa kila aina ya sapoti wakitaka matokeo chanya.

Lengo letu ni kuona wawakilishi wote wanasonga mbele na kutinga hatua ya makundi ili kulinda nafasi ya Tanzania kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo ya CAF kila mwaka, na hilo linawezekana tu kama wawakilishi wetu kila mechi wataichukulia kama fainali. Hivyo, tunawatakia maandalizi mema kuelekea mechi hizo za marudiano kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Simba Queens inahitaji mabadiliko

WAKATI inaondoka nchini kwenda kucheza michuano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati Ukanda wa CECAFA, kuwania tiketi ya timu moja itakayouwakilisha ukanda huo kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa wanawake, Watanzania wengi walidhani kuwa Simba Queens inaweza kabisa kutwaa ubingwa huo.

Ni kwa sababu Simba Queens ilikuwa inatesa mno kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Imetwaa ubingwa mara mbili, lakini ikilitawala soka la Tanzania kwa upande wa wanawake.

Wengi hawakutarajia kile ambacho watakwenda kukutana nacho huko. Mechi ya kwanza ilipata ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya PVP ya Burundi, ikiwa ni mechi ya ufunguzi wa michuano hiyo, Agosti 28, mwaka huu.

Mechi ya pili hali ilibadilika na kulazimishwa sare ya bila kufungana dhidi ya Lady Doves ya Uganda, kabla ya kuachilia kipigo cha mabao 10-0 dhidi ya FAD ya Djibouti.

Simba Queens ikaliongoza Kundi A, ikiwa na pointi saba sawa na Lady Doves na kwenda moja kwa moja nusu fainali.

Hapo ndipo tui na maji vilianza kujitenga. Simba Queens ilitandikwa mabao 2-1 dhidi ya Vihinga Queens ya Kenya, na kuzima kabisa ndoto ya Watanzania wengi kuwa itakwenda kuwakilisha ukanda huu kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kwa upande wa wanawake.

Labda kuna baadhi ya watu walidhani ni bahati mbaya, Simba Queens ilicheza tena mechi ya kutafuta ushindi wa tatu dhidi ya Lady Doves ya Uganda ambao walikuwa nao kwenye kundi moja.

Safari hii hakukuwa na suluhu tena, ikachapwa mabao 2-1 na ikawa ndiyo mwisho wa ndoto ya Simba Queens na Watanzania wote kwa timu hiyo kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kocha Mkuu wa timu hiyo Hababuu Ally alisema wamejifunza vitu vingi kwenye michuano hiyo.

Akasema yanahitajika mabadiliko kwenye kikosi chake, na kwa kuanzia, huenda dirisha dogo ikasajili baadhi ya wachezaji.

Baadhi ya wanachama na mashabiki wa Simba, wameonekana kutoridhishwa na kiwango cha uchezaji wa timu yao hasa kwenye michuano hiyo, wakimtuhumu kocha Hababuu, wakitaka aliyekuwa kocha wa timu hiyo, Mussa Hassan Mgosi, ambaye kwa sasa ni kocha wa vijana chini ya miaka 20 arejeshwe.

Ukiangalia michuano hiyo, utakubaliana kabisa na alichosema Kocha Mkuu wa Simba Queens.

Kwenye Ligi ya Tanzania kwa wanawake, timu nyingi bado ni dhaifu, hivyo Simba ambayo ina afadhali kidogo, inaonekana ni timu bora, lakini kwa tulioangalia michuano hiyo ya CECAFA, pamoja na kujitahidi kwa kila hali, ilikutana na timu ngumu, zenye wachezaji wa aina nyingine kabisa tofauti na wa Tanzania.

Mfano timu kama Vihiga Queens ya Kenya, ambao ndiyo mabingwa wataenda kuwakilisha Ukanda wa CACAFA, wachezaji wao wengi wana nguvu na kasi, tofauti na wachezaji wa Simba Queens.

Hata Lady Doves, ina wachezaji ambao hawatofautiani na Vihiga Queens. Timu kama CBE ya Ethiopia ambayo imefika fainali ya michuano hiyo, yenyewe haina wachezaji wenye nguvu, lakini wana uwezo mkubwa wa kuchezea mpira miguuni.

Ninavyoona kwanza kabisa Simba Queens kwa kusajili kipa. Mfano makipa wa Vihiga Queens na Lady Dives wana uwezo mkubwa mno, kuliko wa Simba.

Pili nafasi ya beki wa kati, nne na tano, isajili wachezaji kama wale tuliowaona kwenye vikosi vya Vihiga na Lady Dives kwani walikuwa na uwezo wa kuruka vichwa juu, warefu na wana nguvu, pia uwezo wa kupambana.

Sehemu ya kiungo, Simba inatakiwa ipate wachezaji wawili au watatu kama wa CBE, ambao wana vipaji na wanyumbulifu, wanaoweza kumsaidia Mawete Musolo, ambaye kuna wakati ilionekana kama yupo peke yake uwanjani na ndiyo msaada pekee wa kikosi.

Sina tatizo sana na sehemu ya ushambuliaji wa Simba Queens, lakini kama inataka kupata mafanikio kimataifa, inabidi ifanye mabadiliko yaliyoainishwa hapo. Na hapo ndipo inaweza sasa kuwaambia Watanzania kuwa inataka kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika.

## Kilimo cha mboga, chawa mkombozi kwa wanawake

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KILIMO cha mboga na matunda katika Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga, kimeleta matumaini mapya ya kiuchumi kwa kikundi cha ujasiriamali cha wanawake cha Lumolumo na kuwafanya waondokane na utegemezi kwa waume zao.

Hapo awali baadhi ya wanawake walilalamika kupigwa na waume zao wanaokwenda kutafuta kipato na kuchelewa kurudi nyumbani, lakini sasa kilimo hicho kimeanza kuwafuta machozi.

Kikundi hicho kilianza kwa kulima nusu hekari ya zao la nyanya na kufanikiwa kupata kiasi cha Sh. milioni nne, hatua ambayo iliwafanya waume zao kutambua mchango wao na kuonekana wanachokifanya kina manufaa kwenye jamii na ndani ya familia wanazotoka.

Hayo waliyabainisha jana wakati wa maadhimisho ya kilele cha Siku ya Mkulima Shambani ambacho kilifanyika Kata ya Segese, Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga.

Kikundi hicho kinafanya shughuli zao kupitia mradi wa kutambua usawa wa kijinsia wa kuwawezesha wanawake na mabinti unatokelezwa na Shirika la TAHA kwa ufadhili wa UN-Women na Koica.

Makamu Mwenyekiti wa kikundi hicho, Angela Paul, alisema kabla ya kupewa elimu ya kilimo cha mboga na matunda walikuwa tegemezi kwenye familia zao na wakati mwingine ilifikia hatua ya kupigwa na waume zao wanapochelewa kurejea nyumbani.

Alisema kwa sasa wanaheshimika baada ya kupata shughuli ya kufanya na kujiingizia kipato cha kaya na hata wakichelewa kurejea nyumbani hawapigwi kama ilivyokuwa hapo awali.

"Halmashauri hii ina zaidi ya vijiji 92 na vijiji vinne ndivyo vinavyonufaika na mradi huu, tunaomba elimu tuliyopata iwafikie na kinamama na mabinti wengine ili kuwakwamua kiuchumi na kupunguza wimbi la mabinti wasiokuwa na shughuli za kufanya mitaani," alisema Angela.

Kwa upande wake, Edina Shigela alisema, wamelima hekari moja ya nyanya na matunda, watakapovuma wanatarajia kupata zaidi ya Sh. milioni 20 na kwamba wataendelea kuzalisha zaidi kwa sababu wana uhakika wa masoko kutoka mgodi wa Bulyanhuru.

Naye Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la Kilimo cha Mboga na Matunda (TAHA), Dk. Jackline Mkindi, alivishauri vikundi vingine kujitokeza kujifunza namna ya kulima kisasa kilimo cha matunda na mboga ili kujikwamua kiuchumi na kuondokana na utegemezi kwenye familia zao.

Alisema licha ya elimu hiyo bado wanawatafutia masoko ya kuuza mazao yao, hivyo kikundi hicho kitapata soko la uhakika la mazao hayo kupitia migodi miwili mikubwa ya Bulyanhuru na Buzwagi na kuwataka kuendelea kuzalisha kwa viwango vinavyohitajika.

Awali Mratibu wa UN Women, Lilian Mwamdanga, alisema lengo wa kuwapatia ujuzi wanawake na mabinti kulima bustani za mboga na matunda ni kuboresha maisha yao pamoja na kutatua vitendo vya ukatili wa kijinsia na tatizo la utapiamlo kwa watoto wadogo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, aliwataka maofisa ugani kuhakikisha wanaorodhesha wakulima wote na kuwaelekeza walime nini kulingana na jiografia ya maeneo yao na kwa kwamba ofisa ugani atakayeshinda ofisini atamchukulia hatua za kisheria.




Washindi wa tuzo ya Tamasha la Fahisi ya Kiswahili katika shule za msingi za Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani, wakiwa na tuzo zao. Katikati ni mshindi wa kwanza Ummy Werema wa darasa la sita, Shule ya Chanzige B, mshindi wa pili Ng'orongo Elia (kushoto) wa darasa la sita Shule ya Chanzige A na mshindi wa tatu ni Denis Mwanga wa darasa la tano katika Shule ya Sanza. Tamasha hilo liliandaliwa na Tanzania Fasihi Fund (TAFF) mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

## DC amaliza utata sehemu za kufanyika biashara

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, amemaliza utata wa maeneo ya kufanyia biashara, baada ya kuwapanga wafanyabiashara wadogo (wamachinga) katika sehemu zinazokubalika na rafiki kwao.

Akizungumzia kuhusu mpango huo, Msando alisema mkakati huo utakuwa endelevu kwa kuwaweka wafanyabiashara wadogo maeneo yaliyokubaliwa ikiwamo katika Soko Kuu la Chifu Kingalu, Manispaa ya Morogoro ili waweze kufanya biashara hizo bila kupata usumbufu.

"Katika zoezi hili tumeamua kuanza na wafanyabiashara ambao wapo kwenye maeneo yasio rasmi na tutawawekea vibanda vizuri vya biashara zao na kupendezesha maeneo yao katika soko letu kuu la Chifu Kingalu," alisema Msando.

Alisema katika hatua ya awali, vibanda zaidi ya 700 vya kisasa vimejengwa eneo la wazi Soko Kuu la Chifu Kingalu, Manispaa ya Morogoro ili kuwapanga wafanyabiashara wadogo maarufu wamachinga ambao wanaendesha biashara zao maeneo yasiyo rasmi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Morogoro mjini kichama, Fikiri Juma alimpongeza Mkuu wa Wilaya kutokana na maono mapya na mtizamo mzuri wa kuona wafanyabiashara wadogo wanapata meneo mazuri ya kufanyia biashara zao. Alisema, hatua ya Mkuu wa wilaya kushirikisha viongozi wengine na wafanyabiashara wadogo kumewezesha utekelezaji wa ujenzi wa vibanda zaidi ya 700 eneo la Soko la Chifu Kingalu.

Alisema kujengwa kwa vitanda hivyo vya kisasa vya biashara kumeweka mazingira mazuri na salama zaidi ya ufanyaji kazi kwa wafanyabiashara hao.

Mwenyekiti huyo wa CCM alisema Mkuu huyo wa wilaya ameangalia wananchi wanataka nini na yeye ni mshirikishaji wa mambo, na kutatua kero hiyo ya muda mrefu.

"Nachukua nafasi hii kumpongeza Rais Samia Suluhu kwa kutuletea Mkuu wa Wilaya Msando ambaye amekuwa mbunifu na mwenye kutumia akili nyingi kuliko nguvu, hawa ndio viongozi tunaowataka," alisema Fikiri.

Alisema, kupangwa katika maeneo rasmi kwa wafanyabiashara hao kutawawezesha kufanya shughuli zao bila bughudha na staha nyakati zote bila kujali jua ama mvua.

Naye mmoja wa wafanyabiashara hao, Salum Mwinchande, alisema zoezi la kuwapanga maeneo mazuri ya kufanya biashara sasa litamaliza mzozo uliokuwa ukijitokeza kutokana na kukosekana kwa sehemu za kufanyia biashara. Alimpongeza Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na Rais kwa kuwawekea mazingira mazuri ya ufanyaji kazi wao bila kubughudhiwa.

Katika eneo la Soko Kuu la Chifu Kingalu, vibanda vimejenga kwa kufuata mistari na kupewa majina ya viongozi wa kitaifa ikiwamo Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na baadhi ya viongozi maarufu wa mkoa huo wakiwamo machifu.

## Taasisi yabaini mwarobaini kuondoa utegemezi kwa vijana

**Na Waandishi Wetu**

TAASISI ya kiraia ya Community Hands CHF imeanzisha mipango wa kuwawezesha vijana kiuchumi kwa ajili ya kuondokana na utegemezi na kuajiri wengine.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Paul Makoe, alisema utafiti wao wa hivi karibuni walibaini changamoto mbalimbali zinazowakabili vijana kiasi cha kushindwa kufikia malengo kwa kukosa maarifa au uwezeshi. Alisema maeneo ya kipaumbele ni elimu, afya, mazingira na kutetea haki za watoto, wanawake na wenye ulemavu hususani viziwi.

"Tuliona kuna uhitaji wa vijana kuwezeshwa kimaarifa, kutokana na matatizo yanayowakabili hususani suala la kukosa ajira, tumekuja na miradi ambayo itaenda kujibu changamoto zao kwa kuwaongezea uelewa na kujua namna ya kujiajiri," alibainisha Makoe.

Aidha, aliongeza kuwa kampuni hiyo inashirikiana na taasisi mbalimbali za vijana pamoja na vyuo vikuu, katika kuanzisha kituo cha ufundishaji mahususi kwa ajili ya kukuza mawazo ya vijana katika ubunifu wanaoufanya ili uweze kuwa na tija.

Aidha, taasisi hiyo pia imelenga kuwainua wanawake kwa kuwapatia elimu ya ujasiriamali itakayowasaidia kujua ni namna gani ya kupangilia matumizi ya fedha katika kuendesha biashara, ili waweze kufikia malengo.

"Katika utekelezaji wa hilo tumeshaanza kuendesha makongamano ya vijana katika Mkoa wa Lindi na Morogoro Vijijini, ikiwa ni moja ya kuiunga mkono serikali katika kuwawezesha vijana kujiajiri wenyewe na kupunguza tatizo la ajira nchini," alisema Makoe.

Alisema tafiti zao zilifanikiwa kubaini uwepo wa uhaba wa vituo pamoja na vifaa vya kufundishia viziwi na wamechukua hatua za awali kutatua kwa kutengeneza programu inayopatikana katika vifaa vya kielektroniki itakayomwezesha mtoto mwenye tatizo hilo kusoma, akiwa mahali popote.

Alisema pia wameshirikiana na Taasisi ya Wezesha Mafanikio, kutoa taulo za kike wanawake kwenye maeneo mbalimbali nchini, ikiwa ni moja ya njia ya kuwasaidia kujisitiri wakati wa hedhi, huku wakiwasisitiza kuwa na utamaduni wa kulinda afya zao.

"Tunaiomba serikali pamoja na wadau na taasisi mbalimbali watuunge mkono kwenye miradi tuliyoianzisha na kuipendekeza ili kufikia malengo ya kuwawezesha vijana wengi zaidi nchini," alisema Makoe.

**Imeandikwa na Maulid Mmbaga (DAR) na Kalebo Mussa (TUDARCo)**

# Mradi kusaidia watoto 700 kutoka familia duni

**NA Francis Godwin,** IRINGA

VIJANA na watoto wanaotoka katika familia duni zaidi ya 700 katika vijiji 16 vya kata za Luhunga, Mdabulo na Ihanu, Wilaya ya Mufindi Mkoa wa Iringa wanatarajiwa kusaidiwa na mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM), kuondokana na tatizo la ugumu wa maisha.

Mradi huo pia umesaidia watoto yatima 51 baadhi yao wazazi wao wamepoteza maisha kwa janga la Ukimwi, kwa kuanzishiwa makazi maalum katika Kijiji cha Igoda, Kata ya Luhunga, Wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa kwa ajili ya kusaidia mahitaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusaidiwa kupata elimu ya msingi hadi chuo kikuu.

Akitoa taarifa hiyo jana kwenye kikao kazi cha mradi huo wa Youth Agency Mufindi (YAM), Meneja wa mradi, Danford Mkumba, alisema mradi huo utasaidia pia kutoa mafunzo yatakayowezesha vijana hao kujikwamua kiuchumi.

Alisema watoto hao wameendelea kupata malezi bora ikiwamo elimu na kuwa pamoja na wenzao kupitia mradi wa YAM vijana na watoto wanaotoka katika familia duni 770 wanatarajia kusaidia na mradi huo kupata elimu ikiwamo ya ufundi wa uselemara kwa watoto wa kike pamoja na kuwapatia vifaa vya kuanzishia viwanda vyao.

Alisema mradi huo upo chini ya Foxes Community and Wildlife Conservation Trust (FCW-CT), unafadhiliwa na Deaconess Foundation ya nchini Finland na kwa Wilaya ya Mufindi mradi huo unatekelezwa chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.

Hata hivyo, alisema mradi huo umepangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka huu na tayari umekwisha andaa wajumbe 160 kutoka vijiji 16 vya kata tatu ikiwamo Ihanu, Luhunga na Mdabulo zote za wilayani Mufindi kuwa mbali ya wajumbe hao kutakuwa na timu ya mradi kutoka Tanzania na Finland, timu ya uwezeshaji kutoka ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, viongozi wa vijiji vyote ambavyo mradi utatekelezwa pamoja na halmashauri zao.

Alisema malengo ya mradi huo ni kuwahusisha vijana wenye ulemavu katika mfumo rasmi wa ajira na ujasiriamali, kuwezesha vijana walio katika mazingiramagumu kujitegemea na kujisimamia wenyewe kutumia fursa mbalimbali zilizopo kwenye maeneo yao.

Pia, kuwaondoa vijana katika tabia zenye athari kwenye maisha yao, kupunguza au kuondoa wimbi la vijana kuhamia mijini kufanya kazi za ndani pia kuleta usawa wa kijinsia katika kuibua na kutumia fursa zilizopo katika jamii.

Alisema mradi huo utaendesha mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana, elimu ya saikolojia, mafunzo maalumu kwa mabinti, mafunzo kwa jamii kuhusu kuwatunza watoto wenye ulemavu na nama bora ya kutumia fursa zinazozunguka pamoja na mafunzo ya kilimo cha mazao ya chakula, kilimo cha miti ya mbao na nguzo za umeme na shughuli nyingine nyingi.

Mwenyekiti wa chama cha watoa huduma za kisaikolojia Tanzania, Dk. Heriel Mfangavo, alisema kutokana na ukubwa wa tatizo Halmashauri ya Mufindi kwa kushirikiana na mdau Fox chini ya ufadhili wa Finland wamekuja na mradi wa YAM ili kusaidia jamii Wilaya ya Mufindi.



Mbunge wa Bukoba Vijijini (CCM), Dk. Jasson Rweikiza, akiwaelekeza jambo madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba Vijijini na Kamati ya Siasa ya CCM ya wilaya hiyo, walipotembelea Shule ya St Anne Marie Academy Mbezi Kimara kwa Msuguri jijini Dar es Salaam, ikiwa ni ziara ya mafunzo kwa madiwani hao. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Madiwani Bukoba wafurahia utekelezaji miradi mikakati

**Na Joseph Mwendapole**

MADIWANI wa Halmashauri ya Bukoba Vijijini (CCM), wameipongeza serikali kwa kazi ya ujenzi wa miundombinu na kushauri kasi hiyo iendelee kwenye miradi yote ya kimkakati.

Waliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam walipotembelea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Terminal III, Daraja la Mfugale, Daraja la Nyerere Kigamboni, Reli ya Kisasa (SGR) na Daraja la Tanzanite.

Madiwani hao walikuwa jijini Dar es Salaam kwa ziara ya mafunzo kwa mwaliko wa Mbunge wa Jimbo hilo, Dk. Jasson Rweikiza, pia walitembelea miradi mbalimbali mkoani Dodoma kabla ya kuja Dar es Salaam.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Diwani wa Kata ya Kanyangereko, Joasi Rweikiza, alisema wamejionea wenyewe utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati kama serikali ilivyoahidi kwenye Ilani ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2020.

"Tulikuwa tunasikia tu, lakini kwa ziara hii tumejionea wenyewe na tunakwenda kuwaambia wananchi kwamba serikali ya CCM inatekeleza ilani ya chama kwa vitendo waendelee kuiunga mkono," alisema.

Alisema madiwani wenzake wamefurahishwa kuona uwanja wa ndege mpya kwa namna ulivyojengwa kwa viwango vya kimataifa.

Alisema ujenzi wa barabara ya njia nane kutoka Mbezi kuelekea Kibaha Mkoa wa Pwani umeondoa tatizo la foleni ambalo lilisumbua kwa muda mrefu.

Alisema watu walikuwa wakitumia muda mrefu kutoka jijini Dar es Salaam kufika Kibaha, lakini ujenzi wa barabara hizo umepunguza muda na kwa sasa dakika 20 pekee zinatosha kufika Kibaha. Diwani wa Kata ya Buterankunzi, Gospel Mashongole, alisema wamejifunza kwa vitendo mambo mengi ambayo awali walikuwa wakiyasikia kwenye vyombo vya habari.

"Mfano ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza tulikuwa hatujawahi kuona, lakini leo tumeona wenyewe sasa tunawaambia watu waliokuwa wanabeza kwamba mambo yanafanyika kwa vitendo," alisema.

Alimshukuru Mbunge wa Bukoba Vijijini (CCM), Dk. Rweikiza kwa ziara hiyo ya mafunzo ambayo alisema imewafumbua macho madiwani hao kwa kuwa awali hawakuwahi kujionea wenyewe utekelezaji wa miradi hiyo.

Naye Dk. Rweikiza alisema dhumuni la ziara hiyo ni kujifunza kwa vitendo, walianzia Dodoma na kujifunza mambo mbalimbali yanayofanywa na Bunge. Alisema madiwani hao wamejionea wenyewe utekelezaji mkubwa wa miradi na wameahidi kwenda kuwaeleza wananchi kwamba serikali waliyoiweka madarakani inatekeleza ahadi zake kwa vitendo.

"Miezi mitatu iliyopita kuna Sh. bilioni 1.5 zilitolewa jimboni kwangu kwa ajili ya kukarabati barabara kuna miradi mingi ya maji ambayo inatekelezwa jimboni kwa hiyo serikali inachapa kazi na wananchi waendelee kuiamini," alisema.

# Taasisi ilivyojikita kusaka taulo za watoto wa kike

**Na Christina Haule,** MOROGORO

TAASISI isiyo ya kiserikali inayojihusisha na masuala ya kijamii 'Wezesha Mabadiliko' ya mjini hapa imekusanya taulo za kike za kufua 200 zenye thamani ya Sh. 2,000,000 kati ya 1,000 zinazokusudia kukusanya ili kusaidia wanafunzi wa shule za msingi na sekondari Manispaa ya Morogoro.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Wezesha Mabadiliko ya mjini Morogoro, Lusako Mwakiluma, alisema jana kuwa wanafunzi wengi wa kike wamekuwa wakihudhuria shuleni mara chache kwa mwezi tofauti na wavulana kwa sababu ya kuingia kwenye siku za hedhi bila kuwa na vifaa thabiti vya kujisaidia.

Hivyo Mwakiluma aliiomba serikali, taasisi binafsi na mashirika ya umma kujitokeza kuchangia kuanzia Sh. 10,000 kwa ajili ya upatikanaji wa taulo za kike za kufua ili kuwasaidia wanafunzi wa kike wa shule za msingi na sekondari Manispaa ya Morogoro kwenda shule muda wote.

Alisema wameamua kukusanya taulo za kike 1,000 zenye thamani ya Sh. milioni 10 ambazo zitatumiwa kwa wanafunzi wa kike kwenye shule 23 za kata zilizopo mjini hapa baada ya kufanya utafiti na kubaini kikwazo hicho kwa watoto wa kike.

"Wezesha Mabadiliko imekuja na zoezi la kukusanya mchango wa taulo za kike za kufua kwa ajili ya kuwasaidia mabinti wanaoishi katika mazingira magumu na hatarishi sana," alisema Mwakiluma.

Alisema taulo za kike za kufua zinadumu kwa miezi 18 hadi miaka miwili na kumsaidia mtoto kusoma akiwa katika hedhi salama.

Mwakiluma alisema ukusanyaji taulo hizo ulianza Juni mwakani huu na unatarajia kukamilika mwishoni mwa mwezi huu, ili kuwakabidhi wanafunzi kabla hawajaenda likizo.

Naye Ofisa Rasilimali Watu kutoka Taasisi ya Wezesha Mabadiliko, Rozana Augustine, aliiomba jamii kuona umuhimu wa kuchangia taulo za kike za kufua kwa ajili ya wasichana shuleni, hatua itakayosaidia kusoma kwa utulivu na kupata ufaulu wanaokusudia.

Mmoja wa wanafunzi kutoka Shule ya Msingi Azimio, Manispaa ya Morogoro, Shamsia Shabani, alisema utaratibu wa kuwapatia taulo za kike utawasaidia kujistiri na kuwa na hedhi salama muda wote wa masomo sambamba na kutokosa vipindi darasani.

# Samia afyeka mawaziri

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS Samia Suluhu Hassan amefanya mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri, huku akimteua Stergomena Tax kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mabadiliko hayo yanakuwa ya kwanza kuyafanya tangu aingie madarakani Machi 19, mwaka huu baada ya Rais John Magufuli kufariki dunia Machi 17, mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa jana usiku na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Jaffar Haniu, ilieleza kuwa: "Rais Samia Suluhu amemteua Tax kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, anachukua nafasi ya marehemu Elias Kwandikwa".

Kabla ya uteuzi huo, Tax aliwahi kuwa Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi Kusini mwa Afrika (SADC), baada ya kustaafu aliteuliwa na Rais Samia juzi kuwa mbunge wa kuteuliwa.

Kadhalika, taarifa ilieleza kuwa Rais amemteua Dk. Ashatu Kijaji kuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, akichukua nafasi ya Dk. Faustine Ndugulile, ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Kadhalika taarifa iliongeza kuwa Rais Samia pia ameihamishia Idara ya Habari katika wizara hiyo kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Taarifa hiyo ileleza kuwa Rais Samia amemteua January Makamba kuwa Waziri wa Nishati, akichukua nafasi ya Dk. Merdad Kalemani ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Makamba aliwahi kuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano katika Serikali ya awamu ya nne, na pia Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) katika Serikali ya Awamu ya Tano.

Pia, taarifa ilieleza kuwa Rais Samia amemteua Profesa Makame Mbarawa kuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, akichukua nafasi ya Mhandisi Leonard Chamuriho.

Mbarawa aliwahi kuwa Waziri wa Mawasiliano katika Serikali ya Awamu ya Nne, katika serikali ya awamu ya tano aliwahi kuwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, na Waziri wa Maji.

Vile vile, katika uteuzi huo Dk. Eliezer Feleshi, ameteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kabla ya uteuzi huo alikuwa Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, anachukua nafasi ya Prof. Adelardus Kilangi, ambaye kwa sasa ameteuliwa kuwa balozi.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa; "Mawaziri wateule na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wataapishwa leo majira ya saa tano asubuhi, Ikulu ya Chamwino, jijini Dodoma.



Mbunge wa Bukoba Vijijini (CCM), Dk. Jasson Rweikiza, akiwaelekeza jambo madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba Vijijini na Kamati ya Siasa ya CCM ya wilaya hiyo, walipotembelea Shule ya St Anne Marie Academy Mbezi Kimara kwa Msuguri jijini Dar es Salaam, ikiwa ni ziara ya mafunzo kwa madiwani hao. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Madiwani Bukoba wafurahia utekelezaji miradi mikakati

**Na Joseph Mwendapole**

MADIWANI wa Halmashauri ya Bukoba Vijijini (CCM), wameipongeza serikali kwa kazi ya ujenzi wa miundombinu na kushauri kasi hiyo iendelee kwenye miradi yote ya kimkakati.

Waliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam walipotembelea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Terminal III, Daraja la Mfugale, Daraja la Nyerere Kigamboni, Reli ya Kisasa (SGR) na Daraja la Tanzanite.

Madiwani hao walikuwa jijini Dar es Salaam kwa ziara ya mafunzo kwa mwaliko wa Mbunge wa Jimbo hilo, Dk. Jasson Rweikiza, pia walitembelea miradi mbalimbali mkoani Dodoma kabla ya kuja Dar es Salaam.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Diwani wa Kata ya Kanyangereko, Joasi Rweikiza, alisema wamejionea wenyewe utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati kama serikali ilivyoahidi kwenye Ilani ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2020.

"Tulikuwa tunasikia tu, lakini kwa ziara hii tumejionea wenyewe na tunakwenda kuwaambia wananchi kwamba serikali ya CCM inatekeleza ilani ya chama kwa vitendo waendelee kuiunga mkono," alisema.

Alisema madiwani wenzake wamefurahishwa kuona uwanja wa ndege mpya kwa namna ulivyojengwa kwa viwango vya kimataifa.

Alisema ujenzi wa barabara ya njia nane kutoka Mbezi kuelekea Kibaha Mkoa wa Pwani umeondoa tatizo la foleni ambalo lilisumbua kwa muda mrefu.

Alisema watu walikuwa wakitumia muda mrefu kutoka jijini Dar es Salaam kufika Kibaha, lakini ujenzi wa barabara hizo umepunguza muda na kwa sasa dakika 20 pekee zinatosha kufika Kibaha. Diwani wa Kata ya Buterankunzi, Gospel Mashongole, alisema wamejifunza kwa vitendo mambo mengi ambayo awali walikuwa wakiyasikia kwenye vyombo vya habari.

"Mfano ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza tulikuwa hatujawahi kuona, lakini leo tumeona wenyewe sasa tunawaambia watu waliokuwa wanabeza kwamba mambo yanafanyika kwa vitendo," alisema.

Alimshukuru Mbunge wa Bukoba Vijijini (CCM), Dk. Rweikiza kwa ziara hiyo ya mafunzo ambayo alisema imewafumbua macho madiwani hao kwa kuwa awali hawakuwahi kujionea wenyewe utekelezaji wa miradi hiyo.

Naye Dk. Rweikiza alisema dhumuni la ziara hiyo ni kujifunza kwa vitendo, walianzia Dodoma na kujifunza mambo mbalimbali yanayofanywa na Bunge. Alisema madiwani hao wamejionea wenyewe utekelezaji mkubwa wa miradi na wameahidi kwenda kuwaeleza wananchi kwamba serikali waliyoiweka madarakani inatekeleza ahadi zake kwa vitendo.

"Miezi mitatu iliyopita kuna Sh. bilioni 1.5 zilitolewa jimboni kwangu kwa ajili ya kukarabati barabara kuna miradi mingi ya maji ambayo inatekelezwa jimboni kwa hiyo serikali inachapa kazi na wananchi waendelee kuiamini," alisema.

# Taasisi ilivyojikita kusaka taulo za watoto wa kike

**Na Christina Haule,** MOROGORO

TAASISI isiyo ya kiserikali inayojihusisha na masuala ya kijamii 'Wezesha Mabadiliko' ya mjini hapa imekusanya taulo za kike za kufua 200 zenye thamani ya Sh. 2,000,000 kati ya 1,000 zinazokusudia kukusanya ili kusaidia wanafunzi wa shule za msingi na sekondari Manispaa ya Morogoro.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Wezesha Mabadiliko ya mjini Morogoro, Lusako Mwakiluma, alisema jana kuwa wanafunzi wengi wa kike wamekuwa wakihudhuria shuleni mara chache kwa mwezi tofauti na wavulana kwa sababu ya kuingia kwenye siku za hedhi bila kuwa na vifaa thabiti vya kujisaidia.

Hivyo Mwakiluma aliiomba serikali, taasisi binafsi na mashirika ya umma kujitokeza kuchangia kuanzia Sh. 10,000 kwa ajili ya upatikanaji wa taulo za kike za kufua ili kuwasaidia wanafunzi wa kike wa shule za msingi na sekondari Manispaa ya Morogoro kwenda shule muda wote.

Alisema wameamua kukusanya taulo za kike 1,000 zenye thamani ya Sh. milioni 10 ambazo zitatumiwa kwa wanafunzi wa kike kwenye shule 23 za kata zilizopo mjini hapa baada ya kufanya utafiti na kubaini kikwazo hicho kwa watoto wa kike.

"Wezesha Mabadiliko imekuja na zoezi la kukusanya mchango wa taulo za kike za kufua kwa ajili ya kuwasaidia mabinti wanaoishi katika mazingira magumu na hatarishi sana," alisema Mwakiluma.

Alisema taulo za kike za kufua zinadumu kwa miezi 18 hadi miaka miwili na kumsaidia mtoto kusoma akiwa katika hedhi salama.

Mwakiluma alisema ukusanyaji taulo hizo ulianza Juni mwakani huu na unatarajia kukamilika mwishoni mwa mwezi huu, ili kuwakabidhi wanafunzi kabla hawajaenda likizo.

Naye Ofisa Rasilimali Watu kutoka Taasisi ya Wezesha Mabadiliko, Rozana Augustine, aliomba jamii kuona umuhimu wa kuchangia taulo za kike za kufua kwa ajili ya wasichana shuleni, hatua itakayosaidia kusoma kwa utulivu na kupata ufaulu wanaokusudia.

Mmoja wa wanafunzi kutoka Shule ya Msingi Azimio, Manispaa ya Morogoro, Shamsia Shabani, alisema utaratibu wa kuwapatia taulo za kike utawasaidia kujistiri na kuwa na hedhi salama muda wote wa masomo sambamba na kutokosa vipindi darasani.

HABARI KITAIFA

# Wataalamu: Afrika iweke kipaumbele kwenye misitu

**Na Salome Kitomari**

WATAALAMU wa misitu wamesema kuna umuhimu wa serikali za Afrika, kutoa kipaumbele kwenye raslimali misitu kwa maendeleo endelevu ya jamii na taifa kwa ujumla.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Prof. Raphael Chibunda, wakati wa ufunguzi wa mkutano wa mtandao kwa nchi za Botswana, Gambia, Kenya na Tanzania wa kubadilishana taarifa na uzoefu wa utunzaji na uhifadhi wa misitu kwa kuzingatia Mkataba wa Paris na mchango wa raslimali hiyo kwenye hali ya hewa.

Alisema SUA imekuwa mstari wa mbele kwenye maendeleo ya misitu Afrika kupitia maendeleo ya kisera za nchi katika maendeleo endelevu.

"Katika miongo iliyopita masuala ya mzingira duniani yamekuwa ni yenye athari kubwa kwa misitui barani Afrika hasa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, uharibifu wa ardhi, uchumi wa kijani na malengo ya milenia, inahitaji nguvu ya pamoja kuyashughulikia kwa kuangalia mbinu bora za kwingine, pamoja na utayari wa serikali , jamii, sekta binafsi," alisema na kuongeza;

"Jukwaa la Misitu Afrika (AFF), limekuwa mstari wa mbele kuimarisha uelewa wa utunzaji na hifadhi ya raslimali hiyo kwa kutumia wataalamu kufanya uchambuzi madhubuti wa masuala mbalimbali muhimu."

Kwa mujibu wa Prof. Chibunda, umakini umekuwa kwenye jamii katika masuala ya mabadiliko ya hali ya hewa kwa kutunza misitu, na kwamba ni muhimu serikali za Afrika kutoa kipaumbele kwenye raslimali hizo katika kushughulikia athari za hali ya hewa.

Awali, Katibu Mtendaji wa Jukwaa la Afrika la Misitu (AFF), Prof. Godwin Kowero, alisema lengo la mkutano huo ni kupata mrejesho wa nchi zilivyotekeleza makubaliano ya mkataba wa Paris na namna matokeo ya utafiti yanaweza kutumika kutunza misitu katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

"Utafiti pia umeangazia namna bora ya kushauri kukabiliana na matokeo ya mabadiliko ya tabia nchi kwa wananchi wa kawaida katika maeneo kame, kuna fursa za ujasiriamali huku wakitunza mazingira kuboresha maisha, kuingiza kipato cha nchi na mtu mmoja mmoja," alisema.

Kwa mujibu wa Prof. Kowero, Kamisheni ya Umoja wa Afrika ya AFF, imeangalia namna wanawake na vijana wanaweza kuwezeshwa kiuchumu kunufaika na raslimali katika maeneo yenye ukame



Meneja Msimamizi wa Taasisi ya Elimu ya WIPAHS, Jabbir Rajan (katikati), akigonganisha mikono na wakurugenzi wa kampuni ya kutengeneza na kuunganisha magari ya GF Assembing, Imran Karmal (kulia) na Ali Jawad (kushoto), baada ya kupokea msaada wa vitanda, meza na viti vya kusomea vilivyotolewa na kampuni hiyo, kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum wanaosoma katika shule za tasisi hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mamlaka kuja kufuatilia masoko mazao ya mifugo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ametangaza kwamba serikali itaunda mamlaka itakayoratibu na kusimamia malisho ya mifugo na kuyatafutia masoko mazao yanayotokana na sekta ya mifugo. Ndaki alibainisha hayo kwenye mkutano wa wadau wa mifugo uliomalizika jana jijini Dar es Salaam, na kwamba serikali inajali maslahi ya wafugaji na kwamba itatekeleza mawazo ya wadau wa sekta ya mifugo katika kuboresha sekta hiyo na kutengeneza mazingira bora ya ufugaji, lengo iendelee kutoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya Taifa.

Waziri Ndaki amesema serikali inafikiria kuanzisha mamlaka itakayosimamia malisho na masoko ya mifugo na mazao yake na kubainisha kuwa mamlaka hiyo itafanya bidii kuinua sekta hiyo pamoja, kupunguza migogoro na kuhamahama kwa wafugaji.

"Serikali itaunda mamlaka hii na moja ya jukumu lake kubwa ni kuaangazia malisho na kutafuta masoko ya mazao ya sekta hii ya mifugo," ameeleza Waziri Ndaki.

Amesema aliutumia mkutano huo kuwatia moyo na kuwahakikishia wafugaji kwamba serikali ipo na itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wafugaji kwa kuwa inatambua mchango wao katika maendeleo uchumi wa taifa pamoja na kutengeneza ajira kwa vijana.

Kaimu Mkurugenzi wa Mipango na Utafiti wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Mzee Kilele, ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Frank Nyabundege, aliwahakikishia wadau wa sekta ya ufugaji ushirikianao kutoka TADB, na kwamba mikutano yenye malengo mazuri kama huo, inaipa benki yao fursa ya kujua, kutambua na kuona jinsi gani inaweza kuwafikia wafugaji wengi zaidi ili waweze kunufaika na fursa zitolewazo na benki hiyo. "Hii imekuwa fursa nzuri kwetu kuwapo hapa. Mkutano huu unatoa nafasi kwetu kukutana na wadau wa sekta ya mifugo na nachukua fursa hii kuwahikishia kuwa benki itaendelea kuongeza kasi katika kutoa mikopo pamoja na kuongeza thamani ya mazao ya mifugo ili kuifanya kuwa sekta imara yenye kuleta tija kwa wafugaji wenyewe na katika kuinua uchumi wa taifa," alisema Kilele.

Alieleza kuwa hadi Agosti mwaka huu, benki hiyo imetoa mikopo ya moja kwa moja kwenye sekta ya mifugo yenye thamani ya Sh. bilioni 23.8 na fedha hiyo imewezesha AMCOs 5 kupata ng`ombe wa kisasa na kunufaisha wafugaji 128. Aidha, Kilele alisema benki imetoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 11.8 na fedha hiyo imewezesha ujenzi wa viwanda vinne vya maziwa.

"Kwa kutambua umuhimu wa sekta hii na uhusiano mkubwa wa kati ya sekta ya mifugo na maziwa tuliona ni vyema tutoe mikopo ambayo iliwezesha ujenzi wa viwanda vinne vya maziwa na wafugaji zaidi ya 6,000 wanauza maziwa yao kwenye viwanda hivyo," alieleza Kilele.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wafugaji Wilaya ya Karagwe mkoani Kagera, Jackson Kamkoto, alisema ukosefu wa elimu kwa wafugaji, uhaba wa maofisa ugani, uhaba wa malisho na maji zimekuwa changamoto kubwa zinazowakabili wafugaji na kupendekeza serikali kuunda chombo maalumu kitakachoratibu masuala hayo ili kuongeza tija kwenye sekta ya ufugaji.

# Kikundi chasaidia vifaa tiba corona

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAKATI serikali ikiongeza jitihada za kupambana na ugonjwa wa UVIKO-19, kikundi cha Wana-Makutu (Programu ya Chama) ambacho kinawajumuisha washiriki wa mafunzo ya kwa mujibu wa sheria waliofanya mafunzo mwaka 1989/1990 katika kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa Kikosi 834 KJ Makutupora, wameunga mkono jitihada hizo katika kuleta maendeleo na kupambana na ugonjwa huo.

Kikundi hicho kimewezesha ununuzi wa vifaa tiba na kuvigawa katika Hospitali kuu ya Mkoa wa Dodoma.

Akizungumza baada ya kukabidhi vifaa tiba hivyo, Mwenyekiti wa Wana-Makutu, Mhandisi Phillip Undile Makota, alisema kutokana na umuhimu wa vifaa tiba hivyo, Wana-Makutu wameamua kuunga mkono juhudi za serikali dhidi ugonjwa wa Uviko-19 kwa kuchangia vifaa tiba vyenye thamani zaidi ya Sh. milioni sita, yakiwemo makasha ya barakoa , makasha ya vitakasa mikono na makasha ya gloves.

"Kutokana na utaratibu mzuri tuliojiwekea, tulifanikiwa kukusanya fedha kutoka kwa wana-Makutu na tumeona eneo kubwa la kuanza nalo ni hili la kununa vifaa tiba hivi vitakavyosaidia kwenye jitihada za kupambana na janga hili," alisema Mhandisi Makota.

Mhandisi Makota alimshukuru pia Mkuu wa Mkoa wa huo, Anthony Mtaka, kutokana na ofisi yake kuratibu ziara nzima ya kikundi hicho ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa kuleta matokeo chanya.

Akipokea msaada huo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Dk. Baraka Mponda, alisema msaada huo umefika wakati mwafaka, kwani utasaidia sana kudhibiti maambukizi ya Uviko-19.

# Mkuranga yaona fursa kwenye utalii

**Na Yasmine Protace, MKURANGA**

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, wametakiwa kushirikiana na watendaji wao wa kata ili kuibua fursa za utalii kwenye maeneo yao.

Mbali na kuibua fursa za utalii, pia mapato yatakayokusanywa kupitia utalii na vivutio yataongeza mapato ya halmashauri.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Khadija Ally, katika kikao cha Baraza la Madiwani, na kwamba uamuzi wa kuibua maeneo ya utalii na vivutio vyake unalenga kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan, katika kuutangaza utalii kitaifa na kimataifa," alisema.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mohamed Mwela, alipongeza ubunifu wa utalii na vivutio, huku akiahidi kutoa ushirikiano ili waendelee kuongeza idadi ya makusanyo ya ndani ya halmashauri na kuendeleza miradi ya maendeleo vijijini.

Alisema Mkuranga ina mito, maziwa, bahari na Msitu wa Hifadhi ya Vikindu, vitu hivyo vitasaidia kuleta watalii.

HABARI KITAIFA

# Bil. 300/- kutekeleza mradi wa maji Pwani

**Na Yasmine Protace, MKURANGA**

ZAIDI ya shilingi bilioni 300 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji katika mkoa wa Pwani.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa huo, Abubakari Kunenge, wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa Mkoa pamoja na Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Mkuranga.

"Kamati ya Siasa Mkoa wa Pwani na Kamati ya Siasa Wilaya ya Mkuranga hapa, tumefanya ziara ya kukagua mradi wa maji katika Kijiji cha Mwanambaya kilichoko Kata ya Mipeko Mkuranga," alisema.

Kunenge alisema jumla ya shilingi bilioni 314 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji mkoani humo.

Aliongeza kuwa, mpaka Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) umeshatekeleza miradi ya upatikanani wa maji na kuwafikia wananchi kwa wastani wa asilimia 78.

Ramadhani Maneno, Mwenyekiti wa Kamati ya Siasa Mkoa wa Pwani, aliwataka wananchi kuhakikisha wanaitunza miundombinu ya maji.

"Wananchi muitunze miundombinu ya maji, ikiwamo na kulipa gharama za uendeshaji kwa wakati ili inapotekeo matengenezo ya miundombinu yafanyike kwa haraka," alisema.

Kaimu Meneja wa RUWASA, Maria Malale, alisema mradi wa maji katika Kijiji cha Mwanambaya ulianza kutekelezwa Julai mwaka 2018 na miundombinu ya mradi huo inatarajiwa kusambazwa kwa umbali wa kilomita 39 na gharama zilizotumika ni kiasi cha shilingi bilioni 2.3.

Aliongeza kuwa mradi huo unakadiriwa kuhudumia kaya 800 na mpaka sasa maombi ya kaya yaliyopokelewa kwa ajili ya kuunganishiwa maji ni 71 kati ya hizo tayari kaya 21 zimeshaunganishwa na zinatumia huduma hiyo.

Diwani wa Kata ya Mipeko, Adili Kinyenga, alisema kuwa kuna changamoto ambayo imejitokeza ambapo baadhi ya wananchi wanaounganishiwa maji kwa gharama kubwa, hivyo aliwaomba watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) kurudi ofisi za kijiji na kata na kujadili gharama hizo bila kuathiri watumiaji wa huduma ya maji.



Mshindi wa shindano la 'Kapu la Wana' linalodhaminiwa na bia ya Pilsner Lager, Jackline Minja (kushoto), akipokea zawadi ya kamera kwa mgeni rasmi Ofisa Tarafa wa Manispaa ya Morogoro, Winfred Kipako, aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Morogoro. Jackline alishinda vifaa mbalimbali vya studio za picha vyenye thamani ya Sh. milioni 10.**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ushirika kujenga kiwanda cha vifungashio

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

CHAMA Kikuu cha Ushirika Songea Namtumbo (SONAMCU LTD) mkoani Ruvuma, kimesema kiko katika ujenzi wa kiwanda cha vifungashio.

Lengo la ujenzi huo ni kuhakikisha wakulima wanaondokana na changamoto ya vifungashio vya mazao ya mahindi, ufuta, soya na mbaazi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Meneja wa SONAMCU, Juma Mwanga, alisema licha ya kiwanda hicho kuzalisha vifungashio kwa bei nafuu na upatikanaji rahisi wa vifungashio kwa wakazi wa Ruvuma, pia kitaongeza mapato kwa wananchi.

Mwanga alisema kiwanda hicho kinamilikiwa na wanachama wa SONAMCU kwa asilimia 100 na kinatarajia kugharimu Sh. 3, 983,889, 800 na kwamba mradi huo ulianza mwaka 2020 na kukadiriwa kukamilika ifikapo 2022.

"Kwa sasa SONAMCU inapata bidhaa ya vifungashio kutoka Dar es Salaam, lakini tunatarajia kiwanda kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kuzalisha vifungashio milioni 10 kwa mwaka," alisema.

Aliongeza kuwa kiwanda kinajengwa kwa kutumia mapato ya ndani kwa asilimia 100 mapato ambayo yanatokana na vyanzo mbalimbali vya chama hicho, na kwamba pia chama kitatumia mkopo kutoka taasisi za fedha. SONAMCU LTD inamiliki kiwanda cha tumbaku cha SONTOP, Hoteli ya Angon Arms, maghala, Chuo cha Ushirika na majengo mbalimbali.

Mwanga alieleza zaidi kuwa katika kuhakikisha chama kinajiendesha chenyewe pasipo kutegemea ushuru utokanao na mauzo ya mazao ya wakulima, kina mipango mbalimbali.

"Katika mwaka wa fedha 2022/2023 chama kina mpango wa kununua na kuanzisha mashamba yenye ukubwa wa ekari 3000 ambayo yatatumika kwa shughuli za kilimo hasa yale yanayouzwa kupitia mfumo wa Stakabadhi Ghalani yaani ufuta, soya na mbaazi," alisema Mwanga

Alisema chama kina mpango wa kutafuta masoko ya tumbaku ambapo kwa hali ya sasa uzalishaji wa tumbaku ni tani 500 tu ambapo wakulima wanauwezo wa kulima zaidi ya tani 10,000.

Kwa kushirikiana na Ofisi ya Bodi ya Tumbaku Tanzania, chama kipo katika mazungumzo ya kutafuta wanunuzi wengine wa tumbaku badala ya kutegemea mnunuzi mmoja ambaye ni kampuni ya Premium Active Tanzania LMT.

Kwa mujibu wa Mwanga, kmwaka wa fedha 2022/2023 cha kina mpango kukodisha au kutafuta mbia wa kuendesha miradi iliyosimama kama Hoteli ya Angon Arms pamoja na Chuo cha Ushirika kilichoko Wilaya ya Namtumbo.

Alisema kuwa zipo changamoto ambazo zinawakabili ikiwamo kukosekana kwa elimu yamfumo wa stakabadhi ghalani kwa wakulima hasa katika maeneo ya wilaya za Nyasa, Mbinga na Madaba.

Pia kuongezeka kwa mgogoro wa kimaslahi kwa wafanyabiashara wanaopinga mfumo kutumia wanasiasa ili kuzuia mfumo usifanye kazi.

# Wajasiriamali washinda mamilioni kampeni SBL

**Na Mwandishi Wetu**

WASHINDI wawili wa kampeni ya 'Kapu la Wana' Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kupitia bia yake ya Pilsner Lager, kutoka mikoa ya Morogoro na Njombe wamekabidhiwa vitendea kazi vyenye thamani ya Sh. milioni 10 kila mmoja.

Kupitia kampeni ya 'Kapu la Wana', bia ya Pilsner imetenga kiasi cha Sh. milioni 50 ambazo zitatolewa kwa washindi watano ambapo kila mmoja atajishindia vifaa kwa ajili ya kukuza biashara yake vyenye thamani ya Sh. milioni 10.

Jackline Lola Minja (30) mkazi wa Morogoro Mjini na mmiliki wa studio ya picha pamoja na Rehema Lawrence Mbuya (29) mkazi wa Njombe na mmiliki wa duka la kuuza pemejeo, wamekuwa washindi wa pili na watatu wa kampeni ya 'Kapu La Wana' baada ya mshindi wa kwanza kutoka wilayani Muleba, mkoani Kagera kupatikana na kukabidhiwa zawadi ya Power Tiller mwisho mwa Agosti.

Jackline kutoka Morogoro amekabidhiwa vifaa vya studio ikiwamo kamera, kompyuta, printa na vinginevyo vyenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa ajili ya kupanua biashara yake wakati Rehema akikabidhiwa gari la kubeba mizigo aina ya Carry kwa ajili kumsaidia kupeleka mizigo ya wateja wake.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zawadi kwa washindi hao, meneja chapa wa SBL, Ester Raphael, alisema zawadi zilizotolewa ni mwendelezo wa kampeni hiyo inayolenga kuwawezesha vijana wajasiriamali wapambanaji kufikia malengo yao kupitia Bia ya Pilsner.

"Pilsner, leo inawazawadia wapambanaji wawili vifaa kwa ajili ya kukuza biashara zao. Siku chache zilizopita, tulishuhudia mpambanaji mwingine Privatus Mujuni kutoka Muleba mkoani Kagera naye akiwezeshwa pia. Kampeni bado inaendelea na kila mpambanaji ana nafasi ya kushinda, tuendelee kushiriki," alisema Ester.

Mshindi kutoka Morogoro Jackline Minja alisema changamoto kubwa aliyokuwa akikabiliana nayo ni ukosefu wa vifaa ambapo alikuwa akilazimika kukodi kamera na vifaa vingine kwa gharama kubwa na hivyo kujikuta akishindwa kupiga hatua.

"Nimekuwa nikishindwa kupiga hatua kwa kuwa vifaa vingi ninavyotumia ni vya kukodi. Faida ninayopata ni ndogo sana kwa kuwa kiasi kikubwa kinakwenda kwenye kukodi vifaa. Bia ya Pilsner imefungua kurasa mpya katika maisha yangu maana sasa vifaa ninavyo na sasa ndoto yangu ya kusimama imara zaidi na kusonga mbele inakwenda kutumia. Naishukuru sana bia ya Pilsner," alisema.

Kwa upande wake Rehema kutoka Njombe alisema changamoto kubwa aliyokuwa anakabiliana nayo ni ukosefu wa usafiri wa kufikisha mizigo kwa wateja na kusema gari alilopewa litamsaidai kuimarisha biashara yake na kumfanya asonge mbele kwa haraka zaidi.

"Nina kila sababu ya kuishukuru bia ya Plisner kupitia kampeni ya 'Kapu la Wana' kwa uwezeshaji huu mkubwa kwangu. Gari hili litanifanya niweze kuwahudumia wateja wangu vizuri zaidi kwa kuwafikishia mizigo," alisema

Kwa mujibu wa Ester, shindano hilo ni mahususi kwa ajili ya vijana wapambanaji wanaofanya shughuli mbalimbali kama ukulima, uvuvi, vinyozi n.k. ambao wanatamani kufikia malengo makubwa lakini wanapata changamoto katika upambanaji wao kutokana na kukosa uwezeshwaji hali inayowapungizia kasi ya kufikia malengo yao na mafanikio kwa wakati.

Nipashe
Spotika



KLABU 5 ZILIZOKUWA NA DIRISHA BOVU LA USAJILI EPL 2021-22 UK. 12



Mbappe

Neymar

# SABABU 4 KWA NINI MESSI ATAWIKA ZAIDI YA RONALDO

**LONDON, England**

NYOTA wawili wakubwa ambao mchezo wa soka umewahi kuwashuhudia wamebadilisha klabu msimu huu wa majira ya joto, Lionel Messi akihamia Paris Saint-Germain na Cristiano Ronaldo akirudi Manchester United.

Macho yote yatakuwa kwenye washambuliaji hawa wa kiwango cha juu kabisa duniani kuona ni wapi wanapandisha timu zao mpya kufanikiwa.

Paris Saint-Germain wamefurahia sana dirisha kubwa la uhamisho katika historia ya mchezo huo, wakati wengi waliona dirisha la uhamisho la Man United kuwa bora kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu.

Hapa tunaangalia sababu nne kwa nini Messi atakuwa na msimu bora zaidi wa 2021-22 kuliko Ronaldo, twende sasa...

**#4. Ushindani mdogo**

Kumekuwa na ukosoaji unaolenga Ligue 1 kwa sababu ya ukosefu wao wa ubora, na wakati ukosoaji mwingi umepita, hakuna ubishi kwamba Ligi Kuu Ufaransa haipo kwenye kiwango sawa na Ligi Kuu England.

Utawala wa Paris Saint-Germain kwenye Ligue 1 umefanikwa vizuri. Msimu uliopita ulikuwa mgumu kwao na walishuhudia Lille ikishinda taji la Ligi Kuu.

Wakati huo huo, Paris Saint-Germain imewaongeza kwenye kikosi chao Messi, Gianluigi Donnarumma, Sergio Ramos na Achraf Hakimi.

Kwa sababu ya nguvu ya kifedha ya Ligi Kuu, klabu zinaweza kutumia kwa uhuru zaidi. Katika Ligue 1, itakuwa janga kama Paris Saint-Germain haitashinda taji la ligi msimu huu, wakati kule kwenye Ligi Kuu England angalau klabu tatu zina nafasi ya kutwaa kombe.

**#3. Nafasi kubwa kushinda Ligue 1**

Kama ilivyoelezwa hapo juu, litakuwa jambo la kushangaza kama Paris Saint-Germain itashindwa kubeba taji la Ligi Kuu msimu huu.

Kwenye Ligi Kuu England, kuwasili kwa Ronaldo, pamoja na Raphael Varane na Jadon Sancho, kumesababisha nao kuwa miongoni mwa wanaopewa nafasi ya kutwaa taji.

Hiyo inaweza kuwa si hivyo, lakini ni dhahiri kabisa kwamba Man City na Chelsea wana nafasi nzuri ya kushinda Ligi Kuu msimu huu.

Nchini Ufaransa, hakuna timu inayoweza kukaribia kikosi cha Paris Saint-Germain. Timu za Ligue 1 zinasifika kwa akademi zao na zinaendelea kutoa wachezaji wazuri, lakini nguvu ya matumizi ya PSG inawafanya wawe na nafasi nzuri zaidi ya kushinda Ligue 1.

**#2. Ligi ya Mabingwa Ulaya**

Baada ya Paris Saint-Germain kuwapata Lionel Messi, Sergio Ramos, Achraf Hakimi, Georginio Wijnaldum, Gianluigi Donnarumma na Nuno Mendes msimu huu wa majira ya joto, kunawafanya kuwa na nafasi nzuri zaidi ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ligi ya Mabingwa Ulaya inabaki kuwa ndio ndoto kubwa ya wamiliki wa Paris Saint-Germain, na wamewekeza sana tangu wainunue klabu kutimiza azma hiyo. Walifika fainali ya mashindano hayo mwaka 2020, lakini walifungwa na Bayern Munich kwenye fainali.

Kwa upande mwingine, Man United inatarajia kufikia hatua za mwisho za mashindano hayo, lakini si miongoni mwa wanaopewa nafasi ya kushinda. Vijana hao wa kocha, Ole Gunnar Solskjaer walifika fainali ya Ligi ya Ulaya msimu uliopita, ambayo walifungwa kwa penalti na Villarreal.

**#1. Sapoti nzuri**

Messi ana Neymar na Kylian Mbappe kama washirika wake katika safu ya ushambuliaji pale Paris Saint-Germain, na pia kuna wachezaji kama Angel Di Maria, Mauro Icardi na Julian Draxler.

Nyota watatu Messi-Neymar-Mbappe ni upatina bora zaidi ulimwenguni. Wote watatu wana nafasi kubwa ya kubadilisha matokeo.

Mashabiki wengi wamefurahi kuona Mbappe hajajiunga na Real Madrid msimu huu wa majira ya joto, kwani walisubiri kwa hamu kuona washambuliaji watatu wa kiwango cha dunia wakicheza pamoja.

Wakati huo huo, usajili wa Man United si mbaya. Jadon Sancho alitakiwa kuwa mshambuliaji bora msimu huu, huku tayari walikuwa na Marcus Rashford, Mason Greenwood na Edinson Cavani pamoja na Ronaldo. Hata hivyo, Paris Saint-Germain safu yake ya usajil ni ya kiwango kingine kabisa.

## ISIKUPITE

KWA mwaka huu pekee, mshambuliaji wa Bayern Munich, Thomas Muller ndiye mchezaji mwenye pasi nyingi za mwisho 'assists' (17) katika ligi tano bora Ulaya; Premier League, LaLiga, Bundesliga na Ligue 1, akifuatiwa na Filip Kostic (Eintracht Frankfurt -16), Borna Sosa (VfB Stuttgart - 12), Paul Pogba (Manchester United - 10) na Moussa Diaby (Bayer Leverkusen - 10).



# KLABU 5 ZILIZOKUWA NA DIRISHA BOVU LA USAJILI EPL 2021-22




**LONDON, England**

DIRISHA la uhamisho wa Ligi Kuu England lilifungwa Agosti 31, kwa hivyo klabu sasa zitalazimika kufanya kazi na vikosi vyao vya sasa hadi angalau Januari mwakani.

Timu katika ligi zingine za Ulaya hazikuweza kutumia fedha nyingi kwa sababu ya athari ya kifedha ya janga la COVID-19, lakini Ligi Kuu England iliendelea kutunisha misuli yake ya kifedha, na klabu zilitumia zaidi ya pauni bilioni moja wakati wa usajili.

Hiyo ilifanya wachezaji wengi wa hali ya juu kuwasili kwenye Ligi Kuu England wakati wa msimu wa uhamisho wa msimu wa majira ya joto. Manchester United iliwasajili Jadon Sancho, Raphael Varane na Cristiano Ronaldo, wakati Chelsea ilimchukua Romelu Lukaku na Saul Niguez.

Makala haya yanaziangalia klabu tano zilizokuwa na usajili mbaya zaidi wakati wa dirisha la uhamisho wa wachezaji kipindi cha majira ya joto, hizi hapa...

**#5. Manchester City**

Manchester City ilivunja rekodi ya uhamisho ya Uingereza wakati walipomsajili Jack Grealish kutoka Aston Villa kwa pauni milioni 100. Nahodha huyo wa zamani wa Villa tayari amekuwa na mwanzo mzuri kwa kufunga bao moja na asisti kwenye mechi tatu za mwanzo na Man City.

Hata hivyo, kipaumbele namba moja cha kocha Pep Guardiola kilikuwa kuleta mshambuliaji wa juu na mbadala wa muda mrefu wa Sergio Aguero.

Muargentina huyo aliondoka klabuni hapo msimu huu wa majira ya joto. Hakuna mbadala aliyeletwa, mabingwa hao wa Ligi Kuu sasa wanakabiliwa na matarajio ya kukauka kwa mabao. Guardiola alikuwa na nia kubwa ya kumleta Harry Kane, lakini Mwenyekiti wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy hakuwa tayari kumwachia.

City ilionekana kuwa na uwezekano mkubwa wa kumleta Cristiano Ronaldo kabla ya raia huyo wa Ureno kusajiliwa Manchester United.

Wachezaji Raheem Sterling na Bernardo Silva waliripotiwa kutaka kuondoka Man City msimu huu wa majira ya joto. Lakini klabu hakuidhinisha mauzo kwa yeyote kati yao.

City sasa inaingia msimu bila mfungaji namba moja. Inaonekana wazi Guardiola haamini kama Gabriel Jesus anafaa kuwa namba tisa. Pia wameshindwa kuwaruhusu wachezaji ambao walitaka kuondoka. Kwa hiyo hili linaweza kuwa dirisha la uhamisho ambalo mabingwa hao wa Ligi Kuu England wakalijutia zaidi.

**#4. Liverpool**

Mashabiki wengi wa Liverpool wameachwa wakikasirika na ukosefu wa usajili uliofanywa wakati wa dirisha la uhamisho msimu huu wa majira ya joto.

Kwa upande mmoja, 'Wekundu' hao waliweza kumpata mmoja wa walinzi bora zaidi Ulaya kwa sasa. Walimleta Ibrahima Konate kutoka Leipzig.

Lakini usajili mwingine mpya umekuwa mwembamba, na Liverpool badala yake inazingatia kuwafunga nyota wao wa kikosi cha kwanza kwa mikataba mipya. Jordan Henderson, Alisson Becker, Fabinho, Andy Robertson, Trent Alexander-Arnold na Virgil van Dijk wote wamesaini mikataba mipya na klabu hiyo.

Lakini Liverpool inaonekana kuwa nyepesi katika theluthi ya ushambuliaji, ikizingatiwa kuwa Mohamed Salah na Sadio Mane hawatakuwapo wakati wa Kombe la Mataifa ya Afrika. Mabingwa hao wa zamani wa Ligi Kuu pia hawakuweka kipaumbele kwa mlinzi Alexander-Arnold.

Liverpool pia ilishindwa kuwauza Divock Origi, Takumi Minamino na Nathaniel Phillips ambao bado wapo kwenye vitabu vya klabu hiyo.

Pamoja na Liverpool kushindwa kuimarisha kikosi chao, kuna maana kwamba ukosefu wa kina unaweza kuwaathiri vibaya wakati wa biashara kumalizika kwa msimu wa ligi msimu huu.

**#3. Wolverhampton Wanderers**

Mbwa mwitu hao walionekana wangekuwa vizuri zaidi msimu huu wa Ligi Kuu England. Lakini vipigo vitatu vimeonyesha timu hiyo ilipaswa kuimarika zaidi katika dirisha la uhamisho.

Wolves waliendelea na mwenendo wao wa kusaini wachezaji chipukizi wa Ureno, kwa kumsajili Francisco Trincao kutoka Barcelona. Hwang Hee-chan pia alijiunga kwa mkopo. Raia huyo wa Korea Kusini anaweza kuwa na msaada kwa kikosi hicho kama alivyoonyesha kule RB Salzburg akiwa pamoja na Erling Haaland na Takumi Minamino.

Jambo zuri ni kwamba, Wolves waliweza kuwabakisha Ruben Neves na Adama Traore licha ya kwamba wote wawili walikuwa wakihusishwa na kuondoka. Lakini klabu hiyo ilishindwa kukubaliana na Lille juu ya mpango wa Renato Sanches. Kwa kuongezea, hakuna kati ya Kieffer Moore, Sven Botman au Duje Caleta-Car waliyeweza kumsajili hadi siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili.

**#2. Newcastle United**

Newcastle United haikuwa na fedha nyingi za kutumia, lakini kocha Steve Bruce alikuwa na hamu ya kumsajili kwa mkataba wa kudumu, Joe Willock. Nyota huyo alitua hapo kwa mkopo msimu uliopita na alionyesha kiwango cha kuvutia. Hata hivyo, mkataba wa pauni milioni 22 na Arsenal ulishindikana.

Lakini timu hiyo bado ipo kwenye wakati mgumu na imekosa nafasi ya kufanya maboresho zaidi ambayo yangewafanya kumaliza juu ya nafasi ya 12 ambayo walimaliza nayo msimu uliopita.

Nyota kama Allan Saint-Maximin na Callum Wilson wote wanasumbuliwa na majeraha.

Newcastle pia ilishindwa katika harakati zao za kuongeza mlinzi mwingine wa kati. Walionekana kuwa na nafasi ya kumsajili Mouctar Diakhaby kutoka Valencia, lakini mwisho wa siku ilishindikana. Hamza Choudhury wa Leicester City na Ainsley Maitland-Niles wa Arsenal nao hawakuweza kutua hapo licha ya kupewa nafasi kubwa ya kuwasajili.

Kwa hiyo, msimu mwingine wa mapambano unawaita Newcastle, ambao hatima yao kwenye Ligi Kuu England inaweza kutegemea kiwango cha Saint-Maximin na Wilson.

**#1. Arsenal**

Arsenal ilimaliza dirisha la uhamisho kwa matumizi ya juu, lakini hali ni mbaya pale Emirates baada ya kuanza vibaya kwenye Ligi Kuu England.

Kocha Mikel Arteta na Edu walichagua kuwekeza kwa wachezaji wachanga wakati wa usajili. Biashara ilikuwa ngumu kwa miamba hao wa London Kaskazini.

Klabu hiyo ilifanikiwa kumleta Ben White kutoka Brighton kwa pauni milioni 50 huku pia ikimsajili kwa mkataba wa kudumu, Martin Odegaard. Lakini shughuli zingine zinaibua maswali: Aaron Ramsdale alinunuliwa kwa mkataba wa pauni milioni 30 ili kutoa ushindani kwa Bernd Leno, mwaka mmoja baada ya kuuzwa kwa Emiliano Martinez kwenda Aston Villa kwa bei ya chini.

Granit Xhaka pia alipewa mkataba mpya licha ya kuonekana kuwa njiani kuondoka msimu huu wa majira ya joto. Lakini Arteta alifanikiwa kuwatoa Willian na Hector Bellerin.

Arteta ametumia pauni milioni 140 kwenye dirisha la uhamisho. Lakini maswali bado yanabaki kama kuna yoyote kati ya wachezaji wapya waliosajiliwa kama wanaweza kuiboresha timu hiyo. Mhispania huyo tayari yuko kwenye hatari ya kutimuliwa baada ya Arsenal kupoteza michezo yao ya ufunguzi. Kwa hivyo matumizi yao makubwa msimu huu wa majira ya joto yamemweka kocha huyo kwenye shinikizo zaidi.

## Nukuu

"Sina nia ya mabao, kinachonivutia ni kushinda mataji. Kamwe sitajilinganisha na Ronaldo [Cristiano]– ni mmoja wa wachezaji watatu bora wa wakati wote. Ninajivunia kucheza dhidi yake na ni vizuri amerejea England," S**traika wa Chelsea, Romelu Lukaku, akifurahi kumwona Ronaldo akirudi Ligi Kuu England kukipiga Man United**



"Wao [Manchester United] walikuwa [washindani wa kombe] kabla ya [Ronaldo] kwa maoni yangu. Walikuwa imara hata kabla ya kuwasili kwa Ronaldo. Nadhani atakuwa na athari kubwa, ni bingwa wa kweli. Hufanya mambo kuwa magumu kwetu. Lakini hayatabadilisha malengo yetu," **Kocha Mkuu wa Chelsea, Thomas Tuchel.**



"Hatimaye nilikuwa na likizo ya furaha kutoka siku ya kwanza hadi ya mwisho. Kabla nilikuwa na uchungu na sasa ilikuwa tofauti kutoka mwanzo hadi mwisho. Watoto wangu wanaimba nyimbo za Argentina wakati wote, wanakumbuka fainali dhidi ya Brazil, na kwangu ni jambo la kushangaza kuona jinsi wanavyofurahia hilo, " **Lionel Messi wakati wakisherehekea ubingwa wa Copa America baada ya kufunga hat-trick wiki iliyopita kwenye mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Bolivia ambayo walienda uwanjani na 'Ndoo' hiyo kwa mara ya kwanza tangu waliitwae.**



# WALIOIKIMBIA LIGI KUU NA KUREJEA MSIMU HUU

**Na Adam Fungamwango**

RATIBA ya Ligi Kuu Tanzania Bara imeshatoka. Kila timu sasa inajua itacheza na nani kwenye mechi ya kwanza wa msimu huu wa 2020/21. Kwa sasa timu zote 16 zinajifua kwa ajili ya kuanza kwa kindumbwendumbwe hicho kitanachomalizika Juni mwakani.

Mashabiki wamejiandaa kushuhudia ligi yenye upinzani mkali ambayo huenda haujawahi kushuhudiwa kwa siku za karibuni. Kwanza kabisa ni kwa sababu ya kuongezeka kwa udhamini wa haki za matangazo. Pili ni kutokana na uchache wa timu. Msimu huu zimebaki 16 tu zilizokusudiwa kutoka 20 misimu miwili nyuma, timu 18 msimu uliopita na sasa zipo 16, zote zitacheza mechi 30 tu.

Tatu ni kuhusu usajili, msimu huu karibuni kila klabu imejitahidi kupata wachezaji wazuri, wenye uwezo ambao wanadhani watawasaidia. Kwenye Ligi Kuu msimu huu pia, mashabiki watashuhudia baadhi ya wachezaji ambao walicheza Ligi Kuu Tanzania Bara huko nyuma. Wakaondoka nchini kwenda kutafuta malisho nje ya nchi, ikiwa na maana kucheza soka la kulipwa. Lakini kwa sababu mbalimbali, wameamua au kulazimika kurejea nchini na kusajili tena kwenye klabu zao za awali, au zingine. Kikubwa tu ni kwamba wamerejea tena kwenye Ligi Kuu ya Tanzania Bara na tutawashuhudia tena viwanjani, hawa hapa...



Makambo

**#1. Heritier Makambo - Yanga**

Mashabiki watamshuhudia tena straika wa Yanga, Mkongomani Heritier Makambo. 'Walimmisi' kwa msimu mmoja baada ya kuondoka nchini mwaka 2019 kwenda kujiunga na Horoya ya Guinea. Akacheza kwa msimu mmoja na sasa amerejea na tayari ameshacheza kwenye mechi ya Wiki ya Wananchi dhidi ya Zanaco ya Zambia, akapachika bao, licha ya Yanga kuchapwa mabao 2-1.

Aliichezea Yanga msimu wa 2018/19, akisajiliwa kutoka klabu ya FC Saint Eloi Lupopo, na kufunga mabao 17, kabla ya kutimkia Horoya. Aliondoka kwenye klabu hiyo na amerejea tena kwenye klabu hiyo hiyo ya ligi hii ya Tanzania.

**#2. David Molinga - Namungo FC**

Alipoondoka Makambo kwenye klabu ya Yanga, ilimsajili straika mwingine, David Molinga, alisajiliwa msimu wa 2019/20. Alifunga mabao 11 kwa msimu mzima, licha ya kwamba hakucheza mechi nyingi kama Makambo. Kutokana na kuonekana ana utovu wa nidhamu na kukwaruzana mara kwa mara na viongozi wake, aliachana na klabu hiyo baada ya msimu, akaelekea nchini Zambia kujiunga na Zesco FC. Amecheza kwa msimu mmoja. Molinga, ambaye ni raia wa DR Congo, amerejea tena kwenye Ligi Kuu ya Tanzania. Lakini yeye hajarejea Yanga, ametua Namungo FC.

**#3. Eliud Ambukile - Mbeya City**

Ni straika wa Kitanzania ambaye aliondoka nchini kwa kusajiliwa na klabu kubwa na kongwe Afrika, TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo. Hiyo ilikuwa ni mwaka 2019, akitokea Mbeya City.

Hata hivyo, kinyume cha matarajio ya wengi, hakung'ara sana wala kupata dakika nyingi za kucheza, hadi TP Mazembe ilipoamua kumpeleka kwa mkopo klabu ya Nkana FC ya Zambia.

Kwa sasa amemaliza mkataba wake na amerejea nchini na kujiunga na klabu yake ya zamani, Mbeya City. Hivyo msimu huu.

**#4. Abdi Banda - Mtibwa Sugar**

Beki huyu wa Kitanzania, mara ya mwisho alikuwa kwenye klabu ya Highlands Park ya Afrika Kusini. Na si hiyo tu, wakati anatoka klabu ya Simba kwenda kucheza soka Afrika Kusini, alijiunga na Baroka FC ya nchini humo.

Banda ni beki wa kati wa klabu ya Coastal Union aliyeichezea tangu mwaka 2012 hadi 2014 alipojiunga na Simba. Mwaka 2017, ndipo alipokwenda kucheza soka la kulipwa Sauzi.


Msimu huu amerejea nchini, mashabiki watamuona tena kwenye Ligi Kuu na si Coastal, wala Simba, amejiunga na Mtibwa Sugar.

**#5. Adam Adam - Polisi Tanzania**

Anakumbukwa kuwa alikuwa mfungaji tegemeo kwenye klabu ya JKT Tanzania ambayo kwa sasa imeshuka daraja, aliondoka nchini baada ya kusajiliwa na klabu ya Al Wahida Trip ya Abu Dhabi.

Hata hivyo, amerejea nchini. Nadhani kwa sababu klabu yake imeshuka daraja, amejiunga na Polisi Tanzania.

**JE, WAJUA?**



CRISTIANO Ronaldo ndiye mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa zaidi Manchester United (pauni 510,000 kwa wiki) akifuatiwa na David De Gea (pauni 375,000) na Anthony Martial (pauni 250,000).



# Vyama vya ushirika vyapewa mbinu kujiendesha kibiashara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amevitaka vyama vya ushirika nchini kuacha kujiendesha kwa kutegemea ushuru wa mazao wabuni mikakati ya kujiendesha kibiashara.

Bashe alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na Wakurugenzi wa Bodi za Mazao na watendaji kutoka vyama vya ushirika nchini.

Alisema ipo haja kwa vyama vya ushirika nchini kubadilika katika namna ya uendeshaji wake ili kuacha kutegemea ushuru wa mazao. Alibainisha kuwa vyama vingi vimekuwa havina mipango ya kuwasaidia wakulima kutoka pale walipo kutokana na kukosa mikakati ya kujiendesha kibiashara. "Leo hii unakuta chama kinategemea ushuru wa mazao kujiendesha wakati zipo fursa nyingi ambazo kinaweza kuzitumia ili kujiendesha kibiashara," alisema Bashe.

Alisema, katika nchi nyingine vyama vya ushirika vimetoka siku nyingi katika mfumo huo na hivi sasa vinajiendesha kibiashara na kuwasaidia wakulima wao kupiga hatua.

Aliziagiza Bodi za Mazao mbalimbali nchini kuandaa mikakati ya kila zao namna litakavyochangia kuongeza pato la taifa na kuboresha maisha ya wakulima.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Athony Mtaka, akizungumza na viongozi pamoja waumini (hawapo pichani) kwenye uzinduzi wa hoteli ya kisasa ya Maniyanguru iliyoko Dodoma Makulu mkoani humo juzi, wa pili kushoto ni mmiliki wa hoteli hiyo, Askofu Dk. Livingstone Denis wa kanisa la EAGT Kongwa. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# SUMA JKT kujenga ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la uzalishaji mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT), limeingia makubaliano ya ujenzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itakayogharimu Sh. bilioni 26.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi, akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa kustia saini mkataba wa ujenzi huo, alisema wameamua kuipa kazi SUMA JKT kutokana na nidhamu yake kwenye utendaji kazi.

Alisema pamoja na imani waliyonayo kwa shirika hilo kiutendaji pia anaamini kazi hiyo itakamilika kwa wakati na ubora.

"Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha hizo za ujenzi awamu ya pili ili kuhakikisha Mji wa Serikali Mtumba unajengwa kwa wakati kulingana na maelekezo yake hivyo hatuna budi kulisimamia hilo ili kutimiza malengo ya nchi," alisema.

Naye Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Evaristo Longopa, alisema ofisi hiyo itatoa ushirikiano wa kutosha ili kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa sita ambalo linajengwa Mji wa Serikali Mtumba chini ya usimamizi na ushauri wa kitaalamu kutoka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA).

Kwa upande wake, Meneja ujenzi wa SUMA JKT Kanda ya Kati, Meja Samweli Jambo, aliahidi ujenzi wa jengo hilo utakamilika kwa wakati na kwa viwango vinavyokubalika.

Meja Jambo alisema shirika hilo limejipambanua kwa uwajibikaji wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu ya ujenzi wa majengo mbalimbali ya serikali, mashirika na majengo ya watu binafsi.

## Mifumo ya kielektroniki kutumika ukusanyaji taarifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Maendeleo ya Ushirika imesema itaanza kutumia mifumo ya kielektroniki kwenye ukusanyaji wa taarifa mbalimbali ili vyama vya ushirika vijiendeshe kisasa.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume hiyo, Dk. Benson Ndiege, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika kikao kazi cha wadau wa ushirika wa mikoa mbalimbali nchini.

Alisema kwa sasa ni lazima kuwe na ushirika wa kisasa na kuachana na utendaji kazi wa mazoea na kuwa na ushirika unaogusa makundi yote.

"Lazima tubadilike tuwe na ushirika ambao unawagusa vijana, wazee kinamama na wafanyakazi na makundi yote, wavuvi watu wa habari lazima tusibaki na ushirika wa kizamani hata mifumo yetu lazima iende kisasa. Wewe kama unaendelea kutembelea na makaratasi wenzako wapo kwenye simu wanapata information (taarifa) lazima na sisi tuendane na hali halisi ya nchi yetu jinsi ilivyo."

"Kwa sasa tunachotamani kwa ukubwa ni imani katika vyama vya ushirika watu wasipokuwa na imani hata tupige kelele au tuweke mifumo gani hawatatumia fursa hizo. Unaweza ukaenda kijijini ukapiga shule yako wanakusikiliza wanakwambia miaka kumi chama chetu kilikuwa kinaleta pembejeo, lakini sasa hivi hakuna," alisema.

Aliongeza, "hatuwezi kwenda bila kuleta imani hili ni jukumu letu sote lazima tuanze kwa kujenga imani kwa kuwa waaminifu."

Amesema malengo yao ni kuhakikisha kunakuwa na vyama imara vya ushirika ikiwamo kuviona vyama hivyo vinakuwa na mifuko ya pembejeo ili kujitegemea. "Ni bora kuwa na vyama vichache na sisi tunajikita na kuwa na vyama imara vya ushirika kwa sababu hiyo tunayo malengo ambayo yatatusaidia mojawapo kwenye vile vyama vya mazao tungependa kuona vyama hivyo vinakuwa na mifuko ya pembejeo na sisi tutajenga mazingira jambo hili liende vizuri," alisema.

Hata hivyo, alisema lazima waanze kutoa huduma mbalimbali kwa wanaushirika ikiwamo huduma ya Bima ya Afya ili wanachama waone umuhimu wa kuwa katika vyama hivyo.

"Tunataka kuona vyama vya ushirika vikitumia mifumo ya masoko ni namna gani ya kumsaidia mkulima kuweza kupata soko, Tume ya Ushirika ipo tayari kushirikiana na wadau kuhakikisha wanapata masoko," alisema.

Dk. Ndiege alisema kuna tatizo la wizi katika vyama vya ushirika na kwamba wamejipanga kwa miaka mitano ijayo kuwashughulikia wote ambao wataiba katika ushirika.

"Tumejikita zaidi kuingia katika mifumo ya kieletroniki katika vyama vya ushirika na tayari zoezi hili limeanza na tutatunza taarifa vizuri na tunawaalika wadau kulibadilisha hili. Tunataka mifumo yote wameingia na wanachama wangapi na amepata pembejeo kiasi gani," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania, Theresia Chitumbi, alisema mkutano huo upo kwa ajili ya kuandaa ushirika mpya ambao utaenda kisasa.

"Tupo hapa kuandaa mikakati ya Tume ya Ushirika kwani ni wadau wa ushirika tupo kwa ajili ya kuleta ushirika mpya na hilo ndio lengo la Rais wetu na tumeona nchi nyingi ambazo ushirika umesimama ndiyo wana maendeleo makubwa," alisema. Alisema ushirika wa zamani ulikuwa wa mazao pekee, lakini sasa hivi wamejipanga kuwavuta vijana na kuubadilisha ushirika na uwe wa kidigitali. "Mimi kwa mtazamo wangu tunatakiwa kubadilika tuwe na ushirika wa kidigitali kuliko kwenye makaratasi ukiwa kidigitali kila kitu kinaonekana tumeanza kuwaingiza vijana kwa kufanya mashindano ya insha na wameanza kuujua ushirika ni nini," alisema.







Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kushoto), akisaidiana na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Kituo cha Uyole jijini humo, Dk. Edwin Chang'a, kubeba mkate wa malisho aina ya hey unaozalishwa na kituo hicho kwa ajili ya kukabiliana na matatizo ya uhaba wa malisho kwa wafugaji hasa kipindi hiki cha kiangazi alipowatembelea hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TAKUKURU yatakiwa kuchunguza matumizi mil.7/-

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

KIONGOZI wa mbio za Mwenge wa Uhuru Maalumu Kitaifa, Luteni Josephine Mwambashi, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya kuchunguza matumizi ya Sh. milioni saba zilizotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa na ofisi ya walimu kwenye Shule ya Msingi Igomelo, wilayani humo.

Fedha hizo zilitakiwa zitumike kununua samani mbalimbali kwa ajili ya shule hiyo, lakini mchanganuo wa matumizi yake hauonekani popote licha ya baadhi ya vitu vilivyokuwa vinatakiwa kuonekana vikiwa vimekamilika.

Luteni Mwambashi alitoa agizo hilo juzi baada ya kukagua utekelezaji wa mradi huo ambao ni miongoni mwa miradi ya Wilaya ya Mbarali iliyokaguliwa na Mwenge huo, kwa ujumla ulipitia miradi yenye thamani ya Sh. bilioni nne.

Alisema katika kufuatilia walibaini Sh. milioni 40 za awali ambazo ziliingizwa kwenye akaunti ya shule hiyo kutoka Serikali Kuu zilitumika ipasavyo na nyaraka zake zinaonekana isipokuwa fedha za awamu ya pili ambazo nyaraka zake hazikuonekana popote.

"Sasa nawaagiza TAKUKURU mfanye ukaguzi wa matumizi ya fedha hizi ndani ya siku moja, ili Mwenge wa Uhuru upate taarifa, haiwezekani serikali itoe fedha halafu matumizi yake yasionekane kwenye maandishi, tulitakiwa tuone hata risiti za manunuzi," alisema Luteni Mwambashi.

Akisoma taarifa ya mradi huo wa vyumba vya madarasa na ofisi, Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Protas Mpogole, alisema mpaka sasa mradi huo umegharimu zaidi ya Sh. milioni 47.6 ambazo kati yake Halmashauri ya Mbarali ilichangia Sh. milioni saba.

Alisema awali kabla ya ujenzi wa vyumba hivyo, Shule hiyo ya Msingi Igomelo ilikuwa na uhaba wa vyumba 12 na kwa sasa vimebaki vyumba 10 pekee.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, aliahidi kufuatilia taarifa za ujenzi wa mradi huo, ili kuondoa utata uliobainika na taarifa itawasilishwa haraka kama ilivyoagizwa na kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa.

"Kwa zile taarifa ulizozitaka mapema nikuahidi kwamba utazipata, lakini kwa zile ambazo umetupa wiki moja tutahakikisha unazipata kabla hujatoka katika mkoa wetu, lakini tutahakikisha kila kitu kinakaa sawa na niwaombe watu wangu watoe ushirikiano," alisema Mfune.

Awali akipokea Mwenge huo kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Marwa Lubilya, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema Mwenge wa Uhuru ukiwa mkoani Mbeya utakimbizwa umbali wa zaidi ya kilometa 460.

Alisema utapita katika wilaya zote tano za mkoa huo ambako utaweka mawe ya msingi, kukagua na kuzindua miradi 34 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 14.

# Watumishi washtakiwa madai kutoa lugha chafu

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, Mpokigwa Andimile, amewashtaki kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Vincent Anney, watumishi wa Idara ya Afya wa wilaya hiyo wanaofanya kazi katika hospitali ya wilaya akidai kutoa lugha chafu kwa wagonjwa.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa uwekaji wa Jiwe la Msingi kwenye Jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali hiyo uliofanywa na Mkuu wa Wilaya, Andimile alisema baadhi ya watumishi wa hospitali hiyo wamekuwa wakitoa lugha chafu kwa wagonjwa.

Alisema vitendo hivyo vinasababisha wananchi kukosa imani na Hospitali ya Wilaya na kumwomba Mkuu wa wilaya, Dk. Anney, kushughulikia viendo hivyo ili wananchi warejeshe imani.

"Mgonjwa akifika hospitalini anategemea kufarijiwa, lakini hapa tumekuwa tukikutana na tatizo la baadhi ya watumishi kuwatolea lugha chafu wagonjwa hali ambayo inawakatisha tamaa wagonjwa wetu," alisema Andimile.

Alisema serikali inafanya kila linalowezekana kuboresha huduma za kijamii, lakini watumishi wasiokuwa waadilifu wanaharibu nia njema ya serikali.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Anney, alisema serikali inaendelea kuboresha hospitali hiyo na imetoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya ukarabati wa baadhi ya majengo.

Alisema matatizo mengine yakiwamo ya watumishi katika hospitali hiyo pamoja na vituo vingine vya umma vya kutolea huduma za afya yataendelea kutatuliwa kwa awamu.

# Uharibifu mazingira wahatarisha Mto Songwe

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

MTO Songwe unaomwaga maji yake katika Ziwa Rukwa, uko hatarini kutoweka kutokana na uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za kibinadamu pamoja majanga ya asili ikiwamo mabadiliko ya tabia nchi yanayoikumba dunia kwa sasa.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa jumuiya ya watumia maji wa Bonde dogo la Mto Songwe uliofanyika katika Mji wa Mlowo wilayani Mbozi.

Mgumba alizitaja shughuli za kibinadamu zinazohatarisha mto huo kuwa ni kilimo kisichozingatia uhifadhi wa mazingira, uchimbaji wa mchanga na baadhi ya wananchi kufyatua matofali kwenye kingo za mto huo.

Vilevile, alisema kuna tatizo la ukataji holela wa miti kwenye vyanzo vya mto huo na kusisitiza kwamba endapo hatua za haraka hazitachukuliwa kuna hatari mto huo ukakauka kabisa miaka ya karibuni.

"Mazingira siku zote hayana adabu, ukiyachezea yatakuadhibu tu, huu mto ni muhimu sana kwa maisha yetu na viumbe wengine wanaotegemea maji, zipo shughuli nyingi za maendeleo ambazo zinategemea mto huu kwa hiyo nawasihi tuchukue hatua za kuunusuru mto huu," alisema Mgumba.

Ofisa Maji wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa, Grace Chitanda, alisema mbali na Mto Songwe kuwa hatarini pia ipo mito mingine inayomwaga maji kwenye Ziwa Rukwa ambayo pia iko hatarini kutoweka ukiwamo Mto Zila uliopo katika Wilaya ya Songwe.

Alisema shughuli zinazoongoza kuharibu mito hiyo ni kilimo, ufugaji na uchimbaji wa madini hasa kwa Mto Zila ambao alisema kwa sasa umejaa mchanga unaotoka kwenye maeneo ya machimbo na kusababisha maji kuanza kupotea.

Alisema uharibifu huo wa mito unahatarisha pia uwapo wa Ziwa Rukwa ambalo ni muhimu kwa wananchi wa maeneo yanayolizunguka pamoja na serikali kwa ujumla.

"Tunakoelekea tutakuja tukose maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani pamoja na shughuli zingine za maendeleo, tukumbuke kwamba mwathirika namba moja wa uharibifu wa mazingira ni binadamu," alisema Chitanda.

Mkurugenzi Msaidizi sehemu ya utunzaji wa vyanzo vya maji kutoka Wizara ya Maji, Rosemary Rwebugisa, alisema mikakati ya serikali kwa sasa ni kuhakikisha inashirikiana na wananchi kunusuru vyanzo vya maji kwenye maeneo yote nchini.

Alisema kwa sasa kuna maeneo mengi ambayo chemchemi zilikuwapo zamani zimepotea kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu pamoja na mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema ili kukabiliana na tatizo hilo, serikali imeunda jumuiya 157 nchi nzima kwa ajili ya kushirikisha jamii kwenye ulinzi wa mazingira na vyanzo vya maji.

"Tumetoa kipaumbele zaidi kwenye maeneo ambayo kuna uharibifu mkubwa zaidi, uundaji wa jumuiya hizi ni hatua muhimu sana kwenye ulinzi wa vyanzo hivi, kwa hiyo tutaendelea kuziunda katika maeneo yote," alisema Rosemary.

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa, Mkanjilwa Watson, alisema kabla ya kuanza mipango ya uundaji wa jumuiya ya watumia maji walianza kutoa elimu kwanza kwa wananchi wote wanaoishi karibu na mto huo.

Alisema walitoa elimu na kuhamasisha kwa wananchi katika vijiji 12 vya Wilaya ya Momba pamoja na Mkoa wa Mbeya ambavyo vipo ukanda wa juu wa mto huo.

# DC aiagiza SUZA matengenezo ya vyoo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja, Suzan Peter Kunambi, ameuagiza uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kampasi ya Beit el Ras kuharakisha kuvifanyia matengenezo vyoo vya mabweni ili kuepusha usumbufu kwa watumiaji.

Aliyasema hayo jana huko Beit el ras alipofanya ziara katika chuo hicho kufuatia kupata taarifa kuwa kwa muda mrefu marekebisho ya vyoo hivyo hayajafanyika, hali ambayo inatishia usalama wa afya za watuamiaji.

Alisema hali ya vyoo hivyo si ya kuridhisha, hivyo aliutaka uongozi wa chuo kuhakikisha matengenezo hayo yanamalizika mapema kabla ya chuo kufunguliwa mwezi ujao. "Kwa kweli hali ya vyoo sio nzuri hata kidogo kimazingira, lakini kwa usalama wa afya za watuamiaji...nimepata taarifa kuwa zaidi ya miezi minane ukarabati ulianza, lakini umesita na vyoo vinaendelea kutumika," alisema Suzan.

Alisema serikali ya wilaya haikuridhishwa na hali hiyo na kuwataka viongozi wa taasisi mbalimbali zilizomo katika wilaya hiyo kuwa na utaratibu maalumu wa kusimamia na kufuatilia mikataba wanayoifunga ya ukarabati wa majengo ya serikali ifanyike kwa wakati uliopangwa.

Naye Mwalimu wa chuo hicho, Asha Mhehe, alikiri kuwa vyoo hivyo haviko katika hali nzuri na ya kuridhisha na havifai kwa matumizi na kuomba uongozi wa chuo kufanya haraka kumaliza matengenezo.

"Tunajua vyoo viko katika hatua ya matengenezo kwa hivyo havitakiwi kutumika hadi pale utakapomalizika ukarabati, lakini kwa sasa naona matengenezo yamesita kwa muda na hatuna taarifa kamili ya kusita kwake," alisema Mhehe.

Kwa upande wake uongozi wa SUZA ulieleza kuwa wamekusudia kuyafanyia ukarabati majengo yake katika kampasi mbalimbali yakwamo madarasa, majengo ya utawala na vyoo.

## Rais Mwinyi amlilia Jaji Haji

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametoa salamu za rambirambi kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki kufuatia kifo cha Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, Haji Omar Haji.

Jaji Haji alifariki dunia juzi katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja Zanzibar na kuzikwa Shakani, Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja.

Katika salamu hizo za rambirambi, Rais Dk. Mwinyi alisema amepokea kwa mshtuko na huzuni kubwa taarifa ya kifo cha Jaji Haji Omar Haji.

Aidha, kupitia salamu hizo za rambirambi, Rais Dk. Mwinyi alimwomba Mwenyezi Mungu kuwapa moyo wa subira na uvumilivu katika kipindi hiki kigumu cha msiba, familia, marafiki, ndugu pamoja na wafanyakazi na viongozi wote wa Mahkama Kuu ya Zanzibar.

Salamu hizo ziliendelea kumwomba Mwenyezi Mungu kumpa rehema na kumjaalia makaazi mema peponi.

Marehemu Jaji Haji Omar Haji aliteuliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar Februari 01 na kuapishwa Februari 08, mwaka huu.

Aidha, Agosti 16, mwaka huu marehemu Jaji Haji Omar Haji aliteuliwa na Jaji Mkuu wa Zanzibar, Jaji Omar Othman Makungu, kuwa Jaji mkazi Kisiwani Pemba.




Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahemd Mazrui (kulia), akimkabidhi Mjumbe wa Shirika la Italian Agency Development Cooperation, Devide Bonechi, kitabu maalum cha kumbukumbu za picha za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar ofisini kwake Mnazimmoja, Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Italia kusaidia Zanzibar katika sekta ya afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amesema Serikali ya Italia ina mpango wa kuisaidia Zanzibar katika sekta ya afya.

Aliyasema hayo juzi, alipokutana na ujumbe kutoka Serikali ya Italia, uliofika Zanzibar kwa lengo la kutathmini namna bora ya kusaidia uimarishwaji wa huduma za afya nchini.

Alisema ujumbe huo kutoka Shirika la Italian Agency Development Cooperation, umelenga zaidi katika kusaidia huduma za uzazi, ili kuhakikisha afya bora ya mama na mtoto inaimarika hasa wakati wa kujifungua.

Alieleza kuwa, shirika hilo linafanya kazi katika nchi za Afrika Mashariki, hivyo wameamua kufika Zanzibar ikiwa ni moja ya maeneo muhimu, ambayo yanahitaji huduma bora za afya katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Mazrui aliwaeleza wageni hao kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ipo tayari kutoa ushirikiano kwa washirika wote wa maendeleo, hasa katika sekta ya afya, ili ustawi mzuri wa jamii uweze kufikiwa kwa haraka.

Alisema uimarishwaji na upatikanaji wa huduma bora za afya Zanzibar, ni chachu ya kuchochea wawekezaji duniani kuwekeza nchini.

"Tunapokuwa na huduma bora za afya hata wawekezaji watakuwa wengi na huduma bora za afya zinavuta uwekezaji na kuwaondolea hofu pale wanapopata tatizo la kiafya, hivyo ugeni huu utasaidia katika kufikia lengo la kuimarisha huduma bora za afya," alisema Mazrui.

Aidha Mazrui alisema kutokana na idadi ya watu kuongezeka kila baada ya muda hasa katika maeneo ya mjini, ipo haja ya kujenga hospitali nyingine katika eneo la mjini ili kupunguza msongamano katika Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja, na kuwapa wepesi kinamama wanaofika hospitalini hapo kujifungua.

Waziri huyo aliipongeza serikali ya Italia kwa kuunga mkono jitihada za kuimarisha sekta ya afya Zanzibar kwa maslahi ya wananchi wote.

Kwa upande wake mwakilishi kutoka Shirika la Italian Agency Development Cooperation, Davide Bonechi, alisema shirika hilo lina mpango wa kuwapa mafunzo madaktari, kusaidia utoaji wa huduma bora za uzazi pamoja na upatikanaji wa vifaa ili kuimarisha huduma za uzazi nchini.

Alisema bado wanaendelea kufanya tathmini kwa kutembelea vituo mbalimbali vya afya Zanzibar katika vitengo vya uzazi ili kuona namna nzuri ya kusaidia huduma hizo.

Alisema mradi huo unaotarajiwa kufanyika kwa muda usiopungua miaka mitatu, utasaidia katika kuimarisha huduma bora za afya Zanzibar, hasa kwa wajawazito.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Fatuma Mrisho, alisema serikali ina mpango wa kupunguza msongamano kwa wagonjwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ili wananchi wapate huduma bora.

Alieleza jitihada za kuimarisha vituo vya afya katika ngazi ya wilaya na mikoa zinaendelea ili kuhakikisha huduma bora mjini na vijijini zinapatikana.

Alieleza kuwa misaada ya vifaa tiba, ujenzi wa vituo vya afya na ujio wa wataalamu itasaidia katika kuwapatia wananchi huduma bora.

# Mbinu kuingiza mifuko ya plastiki nchini yafichuliwa

**Na Christina Mwakangale**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema likiwa katika mkakati wa kuwadhibiti na kuwakamata wafanyabiashara wanaoingiza mifuko ya plastiki hasa vifungashio, limebaini bidhaa hizo huingia nchini kutoka nje, kwa njia zisizo halali.

Limesema mara nyingi limekuwa likikuta bidhaa hizo ziliopigwa marufuku nchini zimo sokoni, na kwamba njia za panya hutumiwa na wafanyabiashara hao kupitia bandari bubu zilizopo fukwe za bahari na ziwani.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, akizungumza na Nipashe mkoani Dar es Salaam kuhusu sula hilo, alisema, kuna vikwazo vingi katika kupambana na wahalifu wanaoingiza bidhaa hizo nchini, hivyo aliomba ushirikiano kutoka kwa jamii na taasisi za umma.

"Suala la plastiki ni changamoto na tunaiomba jamii iweze kushirikiana na sisi, kupambana na wahalifu. Tuna wahalifu wengi sana ambao wanaingiza hizo taka hasa vifungashio vya plastiki kutoka nje ya nchi.

"Wanapita kwenye njia za panya na NEMC hatupo kila mahali, mara nyingi tunashtukia bidhaa ipo sokoni, tukianza kufuatilia tunakuta hizo bidhaa zimepita kwenye mipaka ya kawaida, zinapita kwenye maziwa, bahari. Tunahitaji juhudi ya pamoja kutoka TRA, TBS, Polisi, TAKUKURU, Uhamiaji," alisema Dk. Gwamka.

Alisema ingawa sheria ipo wazi unahitajika ushirikiano na sio kuliachia baraza kupambana na suala hilo, kutokana na uchache wa rasilimali walizonazo na kuhitaji msaada kutoka mamlaka husika.

"Vifungashio vilivyokithiri zaidi ambavyo havijakidhi viwango ni ambavyo vinatumika sokoni kufungashia mtu anaponunua bidhaa fulani," alibainisha Dk. Gwamaka.

Aprili 8, mwaka huu, NEMC ilitoa tamko la kuwakumbusha watumiaji na wauzaji wa mifuko ya plastiki kwamba, hiyo ni tarehe ya mwisho wa matumizi hayo, hivyo ni vyema jamii kuanza kutumia vifungashio mbadala.

Dk. Gwamaka alibainisha kwamba, kwa ambao watakiuka katazo la matumizi ya mifuko hiyo, adhabu yake ni pamoja na faini ya kuanzia Sh. 30,000 hadi 200,000 kutegemeana na kosa.

Pia, alisema kuwa wazalishaji wakubwa wa bidhaa za vifungashio vya plastiki ikiwamo viwanda adhabu ni faini ya shilingi milioni tano hadi Sh. bilioni 10 kutegemeana na aina au ukubwa wa kosa.

"Desemba 31, mwaka jana, NEMC, tuliikumbusha kuhusu kanuni kwamba ilisema vifungashio ambavyo havijakidhi vigezo visionekane katika mazingira. Ili kwa wanaotumia vifungashio na kutengeneza kwa wingi wasajiliwe au kupewa maelekezo," alibainisha.

Alisema lengo la kanuni na katazo hilo ni kulinda mazingira na kuwa endelevu kwa manufaa ya vizazi vijavyo na kupunguza uchafuzi kutokana na mifuko ya plastiki ambayo haiwezi kurejelezwa na haiozi isiyooza ardhini kwa takribani miaka 400 hadi 500.

"Tusiishi kama sisi ndio kizazi cha mwisho katika hii dunia, kwa kuchafua mazingira kana kwamba hakuna viumbe wengine baada ya kizazi hiki, tumeikuta ardhi safi na sisi tunaiacha chafu, si sahihi," alisema Dk. Mafwenga.

TAMKO LA MARUFUKU

Mei mwaka 2016, serikali ilitoa tamko la kupiga marufuku utengenezaji, uagizaji, usambazaji na utumiaji wa mifuko ya plastiki nchini mwishoni mwa mwaka huo, zuio hilo litahusisha bidhaa zinazofungashwa katika mifuko hiyo ikiwamo pombe kali maarufu kama 'viroba'.

Hatua hiyo ni baada ya Bunge lililokaa Septemba mwaka 2016, kufanyia marekebisho Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira wa kipindi hicho, January Makamba, alisema mifuko ya plastiki inachafua zaidi mazingira hasa katika vyanzo vya maji, fukwe za bahari na maeneo ya wazi na kwamba tathmini iliyofanywa na wizara ilibaini vyanzo vya maji kama mito mikubwa, ikiwamo Ruaha, Wami, Pangani, Rufiji, Ruvu na itakauka ndani ya miaka mitano ijayo, kutokana na uharibifu.



Mkuu wa Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Judith Nguli (kulia), akizungumza kwenye kikao cha Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya wilaya hiyo, mjini Liwale, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC Songwe ahimiza wafanyabiashara kulipa kodi

**Na Mwandishi Wetu, SONGWE**

MKUU wa Wilaya ya Songwe, Simon Simalenga, amewahimiza wafanyabiashara wilayani humo kulipa kodi kwa wakati na kutumia mashine za kutolea risiti za kielektroniki (EFD) ili mapato yanayopatikana yachangie kuboresha miundombinu na huduma za jamii wilayani humo.

Simalenga aliyasema hayo alipokuwa akifunga semina ya mabadiliko ya sheria za kodi kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2021 iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Wilaya ya Songwe ipo kilomita 155 kutoka mji wa Vwawa ambao ndiyo makao makuu ya mkoa wa Songwe. Simalenga alisisitiza kuwa hatakuwa na urafiki na wafanyabiashara ambao hawataki kulipa kodi na kuwataka wafanyabiashara wote wafanye biashara zao kwa amani ila walipe kodi stahiki kwa wakati.

"Rais Samia Suluhu Hassan ametutuma kuweka mazingira tulivu na rafiki ya kufanyia biashara, tusiwabughudhi wafanyabiashara, kwa hiyo tusilazimishane tufike mahali tushindwe kuelewana kwa sababu tu hulipi kodi," alisema.

Pia alisisitiza wafanyabiashara kutoa risiti za kielektroniki za EFD badala ya kompyuta ambazo hazijaunganishwa na mtandao wa TRA na kuwaonya wafanyabiashara wanaotoa risiti hizo kuacha mara moja.

Alisema kodi inayokusanywa na TRA ndiyo hiyo inayopelekwa kwao ili kutekeleza miradi ya kimaendeleo kwenye wilaya.

"Ukisikia kuna bilioni kadhaa zimeletwa na serikali kuu, ndiyo hiyo inayokusanywa na TRA. Rais ametupa Sh. bilioni 250 tunajenga kituo cha afya hapa wilayani," alisisitiza.

Awali, akifungua semina hiyo, Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Richard Kayombo amesema, adhma ya TRA ni kuhakikisha kuwa elimu ya kodi inawafikia wafanyabiashara na Watanzania kwa ujumla na wanatoa elimu hiyo katika mikoa yote kwa kuzingatia kuwa kumekuwapo mabadiliko ya sheria za kodi kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2021.

Kayombo amesema pamoja na kuwa lengo la semina hizi ni kufahamiana, kuelimishana na kusikiliza maoni kutoka kwa wafanyabiashara, kubwa zaidi ni kujenga uelewa wa mabadiliko ya sheria za kodi kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2021.

"Ni wajibu wenu kulipa kodi kwa wakati huku TRA tukiendelea kufanya maboresho katika huduma zetu," alisema Kayombo.

Semina za mabadiliko ya sheria za kodi kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2021 zinafanyika katika mikoa yote nchini ikiwamo mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikijumuisha Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi.

## Dar24 yafagiliwa kwa ushindi EJAT

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT) limeipongeza televisheni ya mtandaoni ya Dar24 Media, kwa kuwa televisheni ya kwanza ya mtandaoni isiyo na chombo cha habari cha kawaida (traditional media), kushinda tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari (EJAT-2020).

Baraza limeeleza kuwa hatua hiyo ni mabadiliko kwa mlengo wa vyombo vya habari vya mtandaoni.

Tuzo hizo zilitolewa na MCT katika hafla iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, ambapo mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu wa zamani, Jaji Joseph Warioba.

Ofisa Programu wa MCT, Paul Malimbo, alisema Dar24 Media imeonyesha kuwa vyombo vya habari vya mtandaoni hususan vinavyoweka maudhui ya picha jongevu vinaweza kufanya kazi nzuri inayozingatia maadili na ubora unaotakiwa katika tasnia ya uandishi wa habari.

Katika tuzo hizo, Mtangazaji wa Dar24 Media, Stanslaus Lambat, alitajwa kuwa mshindi katika kipengele cha Uandishi wa Habari za Jinsia na Watoto, kupitia kipindi cha 'On The Bench'.

"Tumeona sasa vyombo vya mtandaoni vimeanza kuja juu, wanafanya kazi kama waandishi wa habari wanaoheshimu maadili, tunaona vinakuja juu, na Dar24 imeonyesha hilo pia. Kwa sababu tumezindua za Mwaka 2021, tunawahamasisha waweze kuleta kazi zenye ubora na zilizopitiwa na wahariri," alisema Malimbo.

Aidha, mwandishi wa habari mkongwe ambaye amewahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Bahi na Mvomero, Betty Mkwasa, alisema televisheni za mtandaoni kwa sasa zinajitahidi kuzingatia maadili na miiko ya uandishi wa habari, na imekuwa chanzo cha kutoa taarifa kwa uharaka.

Adrian Nicholaus Mgaya wa Mlimani TV ndiye aliyeshinda tuzo ya EJAT ya jumla, akiwashinda washindani wake watatu katika kipengele hicho.

HABARI KIMATAIFA

# Chad yatafuta msaada wa pesa nchini Qatar

**N'Djamena, CHAD**

RAIS wa Baraza la Jeshi la Chad, Mahamat Idris Déby, alisafiri jana hadi nchini Qatar, kwa ziara ya siku kadhaa.

Jenerali Mahamat Idris Déby anatarajia kukutana kwa mazungumzo na Emir Tamin Ben Hamad Al-Thani.

Mawaziri kadhaa tayari wako Doha kwa mazungumzo. Chad inategemea Qatar kuisaidia kifedha, pia inaweza kuchukua jukumu katika mchakato wa kisiasa.

Miongoni mwa mawaziri ambao tayari wako Doha, ni Chérif Mahamat Zène, Waziri wa Mambo ya Nje, na yule wa fedha, Tahir Hamid, wamekuwa wakifanya mazungumzo tangu siku ya Alhamisi.

Chad inahitaji pesa kufadhili gharama za kipindi cha mpito na mazungumzo ya kitaifa. Kitita ambacho serikali inahitaji ni Faranga za CFA bilioni 841, sawa na euro bilioni 1.3.

Hata hivyo, Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF), wiki hii uliwataka wadai binafsi wa nchi hiyo kushiriki katika urekebishaji wa deni na Qatar ni mwanahisa mkubwa wa Glencore, kampuni ya Uswisi ya madini ambayo inamiliki visima vya mafuta nchini Chad na inaongoza kundi la wakopeshaji ambalo Ndjamena inadaiwa zaidi ya euro bilioni moja.

Suala lingine, majadiliano na makundi ya kisiasa yenye silaha. Kiongozi wa kundi la waasi la UFR Timan Erdimi, anaishi Qatar tangu mwaka 2009. Kulingana na kiongozi wa kundi hilo, kwa mujibu wa ofisa wa Chad, hakuna mawasiliano yoyote yaliyofanyika kwa sasa.

Mahamat Idriss Déby ameahidi kuendelea kwenye njia ya maridhiano na amefanya siku kadhaa huko Amdjarass, mashariki mwa nchi. Ni ngome ya jamii ya Zaghawa ambayo wanatoka, inasemekana wawili hao ni binamu.

**RFI**



Kiongozi Mkuu wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, akisalimiana na Waziri Mkuu wa Hungary Viktor Orban, wakiwa eneo la makumbusho ya sanaa Budapest, jana. Ikiwa ni ziara ya kwanza kwa Papa Francis kusafiri nje ya nchi tangu alipofanyiwa upasuaji mkubwa wa tumbo, Julai mwaka huu nchini Italia. **PICHA: AP**

# Mjane wa Mugabe Grace kurudi mahakamani Sept. 21

**Harare, ZIMBABWE**

FAMILIA ya Rais wa zamani Zimbabwe, Robert Mugabe, imejipanga kukabiliana na kesi mahakamani, Septemba 21, mwaka huu ikiwa ni zamu ya Grace Mugabe, mjane wa Robert Mugabe kutetea kaburi la mumewe mahakamani.

Grace, anaomba marekebisho ya hukumu ya kiongozi wa jadi wa eneo alikozikwa Robert Mugabe ambaye anaamuru mwili wa kiongozi huyo ufukuliwe na kuzikwa kwenye makaburi ya Mashujaa wa taifa.

Rais Mugabe, alifariki dunia mwaka 2019 baada ya miaka 37 mamlakani, alizikwa katika mji alikozaliwa.

Ingawa, mwezi Mei, kiongozi wa jadi wa eneo hilo, akiombwa na mmoja wakazi wa mji huo, aliamuru mwili ufukuliwe uzikwe katika Makaburi ya Mashujaa wa kitaifa huko Harare.

Kiongozi huyo wa jadi anabaini kuwa mahali pa mazishi hapakuwa pa heshima kulingana na mila. Watoto watatu wa Mugabe wanapinga uamuzi huo.

Watoto hao kupitia wakili Fungai Chimwamurombe, kutoka chama cha mawakili cha Zenas, wanatarajia uamuzi huo wa chifu wa jadi umekumbwa na kasoro nyingi.

Mahakama inawachukulia watoto wa Mugabe kuwa wageni kwa kesi, kwa hivyo, hawana haki ya kukata rufani juu ya hukumu hiyo.

Kuanzia kifo chake Septemba 2019, mazishi ya Robert Mugabe yalizua mvutano mkubwa kati ya familia yake na serikali.

Kambi hizo mbili zilikuwa zikivutana kuhusu mahali pa maziko. Kwa sasa kumeibuka mzozo kuhusu kumbukumbu ya rais huyo wa zamani kulingana na mwanahabari huru Xolisani Ncube.

Mugabe alipinduliwa kwa mapinduzi mnamo 2017. Na alipokufa, serikali ilipambana ili kuweza kumzika Robert Mugabe kwenye makaburi ya Mashujaa wa taifa.

**RFI**

## FBI yaweka hadharani uchunguzi wa Septemba 11

**Washington, MAREKANI**

SHIRIKA la Ujasusi wa Ndani la Marekani (FBI), limeweka hadharani nyaraka za uchunguzi wa mashambulizi ya Septemba 11, kuhusu tuhuma za msaada wa Saudi Arabia kwa washambuliaji kufuatia amri ya Rais Joe Biden.

Jamaa wa waathirika wa mashambulizi hayo walikuwa wamemtaka Rais Biden kutohudhuria mikusanyiko ya kumbukumbu ya miaka 20, iliyofanyika mwishoni mwa wiki, endapo hakuziweka hadharani nyaraka ambazo wanaamini zingelionyesha kwamba mamlaka ya Saudi Arabia zilisaidia hujuma hiyo kutendeka.

Sehemu ya waraka huo wenye kurasa 16 uliotolewa jana, unabainisha mawasiliano baina ya watekaji nyara na washirika wao wa Kisaudi, ndani yake hamna ushahidi wowote kwamba serikali mjini Riadh ilihusika na mashambulizi hayo yaliyoua takribani watu 3,000.

Kwa muda mrefu, Saudi Arabia imekuwa ikisema kwamba haihusiki kwa namna yoyote na mashambulizi hayo.

Ubalozi wa nchi hiyo jijini Washington, haukujibu ombi la kuzungumzia uwekwaji huo hadharani wa nyaraka za siri za uchunguzi wa kijasusi, kwenye taarifa yake ya Septemba 8, ubalozi huo ulisema Saudi Arabia daima imepigania uwazi kwenye matukio yanayohusiana na Septemba 11 mwaka 2001 na inafurahia hatua ya kutolewa kwa nyaraka hizo.

"Kama uchunguzi wa zamani ulivyobainisha, ukiwamo wa Kamisheni ya 9/11 na kutolewa kwa kile kiitwacho kurasa 28, hakujakuwapo ushahidi wowote unaoonyesha kwamba serikali ya Saudia ama maofisa wake walikuwa wanajua kuhusu mashambulizi haya ya kigaidi au kwamba walishiriki kwa namna yoyote ile," ulisema ubalozi huo kwenye taarifa yake.

Licha ya kwamba watekaji nyara 15 kati ya 19 walikuwa wanatoka Saudi Arabia, kamisheni hiyo iliyoundwa na serikali ya Marekani haikupata ushahidi kwamba Saudi Arabia, ilifadhili moja kwa moja kundi la kigaidi la Al-Qaeda, ambalo lilikuwa likipewa hifadhi na Taliban nchini Afghanistan kwa wakati huo.

Hata hivyo, ripoti ya kamisheni hiyo haikusema ikiwa watu binafsi na waliokuwa maofisa wa serikali ya Saudi Arabia, walihusika ama la.

Familia za takribani watu 2,500 ya wale waliouawa na zaidi ya watu 20,000 waliojeruhiwa na wawakilishi wa kampuni za kibiashara na za bima wameifungulia mashitaka Saudi Arabia, wakitaka fidia ya mabilioni ya dola.

Licha ya nyaraka za FBI kuivua serikali ya Saudi Arabia na lawama za mashambulizi hayo, Terry Strada, ambaye mumewe Tom aliuawa Septemba 11 na anayewakilisha jumuiya ya familia za waathirika wa mashambulizi hayo, alisema nyaraka zilizowekwa hadharani Jumamosi mwishoni mwa wiki na FBI zinaondoa mashaka yoyote juu ya ushiriki wa Saudia.

"Sasa siri za Wasaudia zipo hadharani na umefika wakati kwa Ufalme huo kubeba dhamana ya maofisa wake kwa kuwaua maelfu ya watu katika ardhi ya Marekani," ilisema taarifa iliyosomwa na Strada.

**DW**

MECHI KALI
HOME
AWAY
EVERTON
1.72 | 3.77 | 4.82
BURNLEY

1
WEKA PESA.
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND

2
WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO



# RONALDO KAONGEZA HAMASA - SOLSKJAER

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ameisifia klabu hiyo kwa kumleta Cristiano Ronaldo ambaye amesema ameongeza ari kwa timu.

Ronaldo alifunga mabao mawili kwenye mchezo wake wa kwanza kwa United wakati 'Mashetani Wekundu' hao wakiibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Newcastle kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, juzi Jumamosi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 raia wa Ureno, ambaye alishinda mataji matatu ya ligi kipindi chake cha kwanza katika miaka sita alipokaa hapo Old Trafford.


United haijashinda taji lolote tangu mwaka 2017, huku pia wakiwa hawajashinda Kombe la Ligi Kuu England tangu mwaka 2013 na Solskjaer amesifia uwezo wa Ronaldo kwenye kikosi hicho.

"Cristiano ameleta hamasa kubwa zaidi kwa timu na kila mmoja hapa anafurahia uwapo wake," alisema Solskjaer.

"Cristiano ni mchezaji wa tofauti na uwapo wake unawafanya wachezaji kuwa kwenye morali ya juu zaidi."

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or amerudi kwenye kikosi hicho huku pia akiungana na sura mpya, Jadon Sancho na Raphael Varane.

# LUIZ ASAJILIWA RASMI FLAMENGO



**RIO DE JANEIRO,** Brazil

DAVID Luiz amekamilisha uhamisho wa kujiungana na klabu ya Brazil ya Flamengo baada ya kuondoka Arsenal mwishoni mwa msimu uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, amerudi nyumbani kwake baada ya miaka 14 wakati alipoondoka pale Vitoria na kwenda kucheza Klabu za Ulaya Benfica, Chelsea, Paris Saint-Germain na Arsenal.

Alishinda mataji 19 kwa kipindi hicho, yakiwamo makombe mawili pale Stamford Bridge, huku akiisaidia Brazil kushinda taji la shirikisho mwaka 2013.

Alikuwa akihusishwa na Klabu kadhaa kubwa tangu alipomaliza muda wake wa kukaa pale Arsenal, Juni mwaka huu.

Luiz amesaini mkataba utakaomweka katika klabu hiyo yenye maskani yake Rio de Janeiro hadi Desemba 2022.

Mlimzi huyo mwenye uzoefu amewasili Flamengo baada ya kusajiliwa kwa mkopo kwa wachezaji, Camilo Duran, Andreas Pereira na Kenedy, wamejiunga wakitokea Manchester United na Chelsea.

## HABARI MICHEZO

LIVE IN PLAY
BET MECHI IKIENDELEA USHINDE.

SPORTPESA APP
CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA




# IBRAHIMOVIC: MIMI NI ZAIDI YA MESSI, RONALDO




**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic anaamini kwamba, yeye ndiye mwanasoka bora zaidi duniani kwa sasa na hakuna mwingine kama yeye.

Wanasoka wengi hawapendi kuzungumzia maoni yao binafsi juu ya ubora wao, huwaacha wapenzi wa soka na wachambuzi mbalimbali kubainisha ni nani alikuwa bora zaidi, au ikiwa wao ni bora zaidi kwa kupima mafanikio yao na tuzo wanazopata katika soka.

Lakini Ibrahimovic ana maoni makubwa zaidi juu ya ubora wake, hasa akijifananisha na nyota Cristiano Ronaldo na Lionel Messi, na amenukuliwa akisema;

"Ikiwa unazungumza juu ya sifa za ndani, sikosi chochote walichonacho, ukiangalia mataji, ndio sikushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Ninajali sana hilo kwa sababu unapofanya mambo kwa pamoja kama timu, basi mafanikio ya mtu mmoja hufuata. Haiwezi kuwa bora ikiwa si ushindi wa pamoja. Je, ninatamani Ballon d'Or?

"Ballon d'Or inanitamani mimi. Katika moyo wangu, nadhani mimi ndiye mchezaji bora zaidi duniani kwa sasa.

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 13 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 2554 | Junior Sevan vs Bkma Yerevan | 1.39 | 4.54 | 6.38 |
| 16:00 | 5876 | Miercurea Ciuc vs Universitatea Cluj | 3.86 | 3.14 | 1.93 |
| 17:00 | 5726 | Maritsa Plovdiv vs Litex Lovech | 1.43 | 4.26 | 6.19 |
| 17:30 | 2264 | FK Zeleznicar Pancevo vs FK Timok 1919 Zajecar | 1.73 | 3.85 | 4.50 |
| 18:00 | 3356 | Farul Constanta vs Clinceni | 1.44 | 4.13 | 7.08 |
| 18:00 | 3491 | FK CSKA 1948 II vs PFC Dobrudzha Dobrich | 1.42 | 4.26 | 6.38 |
| 18:15 | 1403 | Beroe vs Tsarsko Selo | 1.90 | 3.24 | 3.87 |
| 18:30 | 3291 | Rubin Kazan vs Ural Yekaterinburg | 1.67 | 3.54 | 5.12 |
| 19:00 | 2660 | Gornik Leczna vs Wisla Plock | 2.86 | 3.15 | 2.34 |
| 19:00 | 4029 | Stomil Olsztyn vs Resovia Rzeszow | 3.59 | 3.20 | 1.99 |
| 19:00 | 4278 | Urartu vs Pyunik Yerevan | 2.18 | 3.05 | 3.24 |
| 19:30 | 3672 | Veres Rivne vs FK Lviv | 2.00 | 3.34 | 3.38 |
| 19:30 | 5604 | Aris Salonica vs OFI Crete | 1.49 | 3.94 | 6.70 |
| 19:30 | 5898 | Rostov vs FC Krasnodar | 3.26 | 3.50 | 2.07 |
| 19:45 | 5166 | Le Mans vs Sedan | 2.00 | 2.98 | 4.00 |
| 20:00 | 1526 | Balikesirspor vs Tuzlaspor | 4.45 | 3.58 | 1.69 |
| 20:00 | 2238 | Gaziantep BB vs Antalyaspor | 2.27 | 3.31 | 3.01 |
| 20:00 | 2420 | Vasalunds IF vs GIF Sundsvall | 2.95 | 3.55 | 2.27 |
| 20:00 | 2735 | Orebro SK vs Varbergs Bois | 2.76 | 3.20 | 2.38 |
| 20:00 | 2922 | Odense vs Sonderjyske | 1.69 | 3.79 | 4.53 |
| 20:00 | 3155 | Mjallby vs AIK Football | 3.97 | 3.24 | 1.87 |
| 20:00 | 4390 | Turkgucu Ataspor Munchen vs Duisburg | 1.96 | 3.49 | 3.54 |
| 20:00 | 5154 | Alanyaspor vs Giresunspor | 2.00 | 3.40 | 3.55 |
| 20:00 | 5598 | Esteghlal Tehran vs Al Hilal Riyadh | 3.29 | 3.38 | 2.02 |
| 20:00 | 5820 | Elfsborg vs BK Hacken | 2.10 | 3.44 | 3.05 |
| 21:00 | 1058 | Jong Utrecht vs Jong PSV | 2.21 | 3.57 | 2.84 |
| 21:00 | 1418 | Getafe vs Elche | 1.78 | 3.31 | 5.21 |
| 21:00 | 2155 | Hull City U23 vs Swansea U23 | 1.93 | 3.59 | 3.35 |
| 21:00 | 2459 | Maritimo vs FC Arouca | 2.08 | 3.16 | 3.60 |
| 21:00 | 2630 | FC Eindhoven vs Helmond Sport | 2.11 | 3.51 | 3.07 |
| 21:00 | 3062 | FC Volendam vs Roda Kerkrade | 2.09 | 3.70 | 3.20 |
| 21:00 | 3497 | West Bromwich U23 vs Newcastle U23 | 3.04 | 3.76 | 2.00 |
| 21:00 | 3762 | Wigan U23 vs Charlton U23 | 2.18 | 3.49 | 2.86 |
| 21:00 | 3832 | Leicester U23 vs Crystal Palace U23 | 2.19 | 3.78 | 2.67 |
| 21:00 | 4275 | Kfco Wilrijk vs St Truiden | 2.39 | 3.46 | 2.72 |
| 21:00 | 4813 | Jong Ajax vs NAC Breda | 2.40 | 3.76 | 2.49 |
| 21:00 | 5238 | Jong AZ Alkmaar vs De Graafschap | 3.51 | 3.85 | 1.85 |
| 21:00 | 5274 | Universitatea Craiova vs Sepsi Osk | 1.99 | 3.20 | 3.79 |
| 21:00 | 5385 | Ujpest FC vs Zalaegerszegi TE | 1.89 | 3.63 | 3.43 |
| 21:00 | 5404 | Middlesbrough U23 vs Stoke City U23 | 1.82 | 3.78 | 3.54 |
| 21:30 | 2683 | Radomiak Radom vs Pogon Szczecin | 3.00 | 2.95 | 2.36 |
| 21:30 | 5856 | Viseu vs Sporting Farense | 3.52 | 3.17 | 2.06 |
| 21:45 | 1536 | Le Havre vs Toulouse | 3.94 | 3.00 | 2.05 |
| 21:45 | 4897 | Bologna vs Verona | 2.13 | 3.62 | 3.22 |
| 22:00 | 2624 | Everton vs Burnley | 1.72 | 3.77 | 4.82 |
| 22:00 | 3593 | Lugo vs Huesca | 3.59 | 3.00 | 2.16 |
| 22:00 | 4870 | Finn Harps vs Bohemians FC | 3.49 | 3.20 | 2.02 |
| 22:15 | 2328 | Stjarnan vs Hafnarfjordur | 2.18 | 3.57 | 2.80 |
| 23:00 | 1111 | Granada vs Betis | 3.02 | 3.22 | 2.42 |
| 23:15 | 4462 | Tondela vs GD Estoril | 2.85 | 3.19 | 2.44 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# PELE APATA NAFUU BAADA YA UPASUAJI

**SAO PAULO,** Brazil

GWIJI wa mpira wa miguu nchini Brazil, Pele baada ya kuwa kwenye uangalizi wa wagonjwa mahututi, sasa amepata nafuu ya kuridhisha baada ya kufanyiwa upasuaji wa uvimbe wa utumbo mpana.

Mkongwe huyo mwenye umri wa miaka 80, alilazwa katika Hospitali ya Albert Einstein hapa Sao Paulo.

Timu yake ya madaktari ilisema kwamba, alikuwa anafahamu, anazungumza kikamilifu na anaendelea na ishara muhimu za kawaida."

"Kila siku inayopita ninajisikia vizuri kidogo," mshindi huyo wa Kombe la Dunia mara tatu, ambaye amekuwa na matatizo kadhaa ya kiafya hivi karibuni, alisema kupitia Instagram.

Aliongeza kuwa: "Bado nitapona hivi karibuni".

"Wakati niko hapa, ninachukua fursa ya kuzungumza mengi na familia yangu na kupumzika," alisema.

"Asante tena kwa ujumbe wote wa upendo. Tutakuwa pamoja tena hivi karibuni!"

Tatizo linaloshukiwa lilipatikana wakati wa vipimo vya kawaida hospitalini ambapo amekuwa akipatiwa matibabu tangu Agosti 31, mwaka huu.

Pele ndiye mfungaji bora wa muda wote wa Brazil na mmoja wa wachezaji wanne tu aliyefunga katika mashindano manne tofauti ya Kombe la Dunia.

Mapema wiki hii, Lionel Messi alimpita kama mfungaji bora kwa wanaume Amerika Kusini katika mechi za kimataifa na hat-trick katika ushindi wa kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Bolivia.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LUKAKU AFUNGUKA NDOTO KUFUNGA STAMFORD BRIDGE

●●● Nilikuwa na wakati wa kupanda na kushuka kipindi changu cha kwanza, lakini sasa...

**LONDON, ENGLAND**

STRAIKA wa Chelsea, Romelu Lukaku amesema kufunga kwenye Uwanja wa Stamford Bridge ni kitu ambacho alikiota tangu akiwa mtoto mdogo, baada ya kufunga mara mbili wakati Chelsea ikiibuka na ushindi dhidi ya Aston Villa, Jumamosi.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alifunga kwa mara ya kwanza mabao yake kwenye uwanja huo, huku Mateo Kovacic naye akifunga kwa kikosi hicho cha kocha, Thomas Tuchel ambacho kimeendeleza rekodi ya kutopoteza mchezo msimu huu.

"Ni ndoto yangu tangu nilipokuwa na umri wa miaka 11. Nimejitahidi zaidi hasa kwa wakati huu," alisema Lukaku.

Aliongeza: "Nilikuwa na wakati wa kupanda na kushuka mwanzoni (katika kipindi changu cha kwanza), lakini sasa nimeendelea kwa ubora wangu kwa miaka mitatu.

"Kwa uzoefu na kufanya kazi kwa bidii, ninaendelea kujituma kwa bidii.

"Ni mwanzo mzuri, lakini natakiwa kuendelea kujibidiisha. Tunajua kwamba, mwaka huu kutakuwa na ushindani mkubwa.

"Timu nyingi zitapambana kwa ajili ya kuwania taji la Ligi Kuu, hivyo ninaamini ushindani utakuwa mkubwa zaidi."

Lukaku alibusu nembo ya klabu hiyo wakati akisherehekea bao lake la ufunguzi mbele ya mashabiki wa 'Blues' hao baada ya kumfunga golikipa wa Villa, Jed Steer dakika ya 15 kwenye dimba la Stamford Bridge.

Lukaku akafunga bao lake la pili kwa Chelsea na kuihakikisia ushindi.

Ushindi huo ulikifanya kikosi hicho cha Tuchel kushika nafasi ya pili kwenye msimamo nyuma ya vinara Manchester United.

## ZISIKUPITE

### HALAAND HANA HARAKA

MSHAMBULIAJI wa Norway na Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, hana nia ya kuharakisha uamuzi kuhusu hatima yake ya baadaye wakati kifungu cha kumwezesha kuondoka kitaanza kutekelezwa mwaka 2022. **(90 Min)**

### BELLINGHAM AGOMBEWA

MANCHESTER City wamemwongeza Jude Bellingham wa Borussia Dortmund kwenye orodha ya wachezaji wanaowasaka na watamenyana na Liverpool kumpata kiungo huyo wa kati wa England mwenye umri wa miaka miaka 18. **(Star on Sunday)**

### BARCELONA YAMKATAA NDOMBELE

BARCELONA imekataa kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa, Tanguy Ndombele mwenye umri wa miaka 24, na beki wa Ivory Coast, Serge Aurier mwenye miaka 28, kama sehemu ya mkataba wa kumuuza mchezaji wao Emerson Royal kwa Tottenham. **(Fabrizio Romano, via Sunday Express)**

### OVERMARS AIKATAA ARSENAL

MKURUGENZI wa Michezo wa Ajax, Marc Overmars, amesema yuko radhi kutekeleza jukumu lake la sasa katika klabu ya Barcelona badala ya Arsenal. **(Ajax Life, via Marca)**

### ANCELOTTI HANA MAJUTO

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti amesema "hakuna majuto" katika klabu hiyo baada ya juhudi za kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, kutoka Paris St-Germain katika msimu wa majira ya joto kushindikana. **(Goal)**

### LEIGH ATAKIWA WEST HAM

WEST Ham wanamfuatilia kiungo wa kati wa Preston North End, Lewis Leigh huku Everton pia wakielekeza darubini yao kwa mchezaji huyo wa Uingereza mwenye umri wa miaka 17. **(Football Insider)**

### TUCHEL AJUTIA KWA ODOI

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amesema "tulifanya uamuzi wa busara" kutomuacha winga wa England, Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 20, kuondoka siku ya mwisho ya uhamisho wa wachezaji. **(Football London)**

### RODGERS ALENGWA ARSENAL

ARSEAL wanamlenga kocha wa Leicester City, Brendan Rodgers na mkufunzi wa Nice, Christophe Galtier kama chaguo lao endapo wataamua kumfurusha Mikel Arteta. **(Transfer Window Podcast, via Teamtalk)**

### WALLACE LULU ENGLAND

MKATABA wa kiungo mshambuliaji wa Millwall, Jed Wallace unamalizika msimu ujao na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ananyatiwa na Brentford, Burnley, Crystal Palace, Newcastle United, West Ham Pamoja na Celtic, Rangers na West Brom. **(Football League World)**

### ADEYENI AWANIWA CHELSEA

CHELSEA walifanya mazungumzo ya kumsajili kinda matata wa Ujerumani, Karim Adeyemi mwenye umri wa miaka 19, miaka mitatu iliyopita, lakini hawajafanikiwa kumpata mshambuliaji huyo wa Red Bull Salzburg. **(Sunday Express)**

## HABARI MICHEZO

### TSA yatoa vigezo vya mashindano kuogelea

**Na Mwandishi Wetu**

WAOGELEAJI waliofikia viwango vya Kamati ya Ufundi ya Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA), ndio wanaoruhusiwa kushiriki katika mashindano ya wazi ya Klabu Bingwa ya Taifa yaliyopangwa kufanyika kwenye bwawa la kuogelea la klabu ya Gymkhana Septemba 25 na 26, mwaka huu.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya mashindano hayo, Hadija Shebe, katika maohojiano na gazeti hili.

Hadija alisema wameamua kuweka sheria hiyo kwa lengo la kupata washindani wa kweli ili kuwapa nafasi makocha wa timu ya taifa kufanya tathmini ya waogeleaji kwa ajili ya uteuzi wa timu za taifa mahususi kwa mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Alisema hatua hiyo pia italeta ushindani kwa waogeleaji katika klabu zao na kuchagua waliokidhi masharti hayo na kwamba wanatarajia kuwa na waogelaji zaidi ya 150 kutoka klabu mbalimbali hapa nchini.

Shebe alisema katika mashindano hayo yaliyodhaniwa na Samsa Logistics Limited, Sapphire Court Hotel Limited, Selcom Paytech Ltd, Pepsi, Azam, Gymkhana Club, Tarmal Industries Ltd, Tanpack na Flames Restaurant yatashirikisha waogeleaji wenye umri kuanzia miaka tisa na 15.

Alisema kuwa kutakuwa na makundi manne, kundi la miaka tisa na 10, 11 mpaka 12, 13-14, na 15 ambapo mwogeleaji atakayeibuka wa kwanza atapata pointi 20 wa pili na tatu watapata pointi 16 na 14 kila mmoja.



Wafanyakazi wa Benki ya NMB wakiongozwa na Mkuu wa Kitengo cha Mikopo kwa Biashara (NMB Head Wholesale Credit ), Nishad Jinah pamoja na Shangwe Kapinga (katikati), Meneja Mwandamizi Raslimali Watu na Meneja wa NMB Jogging Club, Shadrack Mijjinga, wakifanya mazoezi kwa ajili ya maandalizi ya NMB Marathon-'Mwendo wa Upendo' inayotarajiwa kufanyika Septemba 25, mwaka huu katika viwanja vya Leaders Club ambapo mgeni rasmi atakuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa. **MPIGAPICHA WETU**

# MBIO ZA MAJARIBIO NMB MARATHON 2021 ZAFANA

**Na Mwandishi Wetu**

MAMIA ya wakimbiaji, jana walijitokeza kushiriki mbio za majaribio kupasha misuli na kutambulisha njia zitakazotumika kwenye NMB Marathon 2021, zitakazofanyika Septemba 25, zikilenga kukusanya fedha kwa ajili ya matibabu ya kinamama wenye fistula katika Hospitali ya CCBRT.

Wakiongozwa na wenyeji wao NMB Jogging Club, washiriki wengi binafsi walijitokeza kukimbia mbio hizo katika kategori zote za kilomita tano,10 na 21, kuanzia Leaders Club na kuishia hapo hapo, wakiwamo pia mabalozi wa mbio hizo Efm Jogging na Fanja Jogging.

Akizungumza baada ya kukamilika kwa mbio zote, Nahodha wa NMB Jogging Club, Jesca Sanga, alizishukuru Klabu za Efm, Fanja na wakimbiaji binafsi wote waliojitokeza katika mbio ndogo hizo, huku akiwahimiza Watanzania kutumia vema fursa ya kusogezwa mbele kwa kinyang'anyiro hicho, kujisajili kwa wingi.

"Tuko hapa kushiriki mbio ndogo za kukagua na kutambulisha njia, lakini kupasha misuli moto kuelekea NMB Marathon 2021 'Mwendo wa Upendo.' Hakika zimefana na tunatoa wito kwa Watanzania kujitokeza kushiriki mbio kuu hapo Septemba 25.

"Zimesogezwa mbele ili kutoa fursa kwa wakimbiaji wengi zaidi kujisajili kama walivyoomba, kwa hiyo nitumie fursa hii kuwahamasisha wajitokeze sasa vituoni kujisajili, ili kufanikisha 'Mpango Mkakati' wa kurejesha furaha usoni mwa kinamama wenye fistula kote nchini kama lengo la NMB Marathon lilivyo," alisisitiza Jesca.

Kwa upande wa Mratibu Mwenza wa NMB Marathon 2021, Suleiman Nyambui, alikiri kufurahishwa si tu na wingi wa washiriki wa mbio ndogo hizo, bali pia hamasa na ushindani kutoka kwa washiriki hao, mambo yaliyoonyesha ishara njema kuelekea Septemba 25 ya mbio kuu.

"Kimsingi majaribio yamefana, mwitikio ulikuwa mkubwa, ushindani umeonekana kuwa wa kutosha. Hizi ni ishara kuwa NMB Marathon 2021 itakuwa moto. Kulikuwa na changamoto chache wakati wa majaribio haya, na tunawahakikishia tuliyafanya ili kujua wapi pa kuboresha, mbio kuu hazitakuwa na kasoro yoyote," alisema Nyambui.

Licha ya kuwa NMB Marathon ni mbio za hisani kuchangisha fedha za matibabu ya fistula, lakini zitakuwa na zawadi kwa washindi, ambapo kilomita 21 ambazo ada ya usajili ni Sh. 30,000, bingwa atatwaa Sh. milioni 1.4, wa pili Sh. milioni 1.1 na watatu Sh. 700,000.

Katika mbio za Kilomita 10 ambazo ada ya usajili ni Sh. 20,000, mshindi atachukua Sh. 700,000, wa pili Sh. 500,000 na wa tatu Sh. 300,000, huku kinara wa kilomita tano zawadi yake ni Sh. 250,000, wa pili Sh. 150,000 na wa tatu Sh. 100,000. Ada ya usajili ya mbio za kilomita tano ni Sh. 20,000 na mchakato wa kusajili washiriki wote utafungwa Septemba 25.

# Betway yazindua kituo cha michezo Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Kimataifa ya Michezo ya Kubashiri (Betway), imechukua hatua kubwa katika kuongeza thamani kwenye sekta ya michezo nchini Tanzania baada ya kuzindua kituo cha kisasa cha kushuhudia michezo na kubashiri kistaarabu 'Betway Sports Experience Center'.

Kituo hicho cha kipekee na cha aina yake ambacho kitakuwa sehemu maalum ya kuwakutanisha wapenzi wa michezo kushuhudia michezo mbalimbali na kufanya ubashiri katika mazingira ya kuvutia, kimepewa jina la Dimba la Betway, ambapo kitakuwa pia kikitoa elimu kuhusu michezo na namna ya kubashiri kistaarabu.

Katika kituo hicho ambacho kipo ndani ya ofisi za Betway zilizopo Mbezi Beach, Dar es Salaam, kimewekwa vifaa vya kisasa ikiwamo simu janja na kompyuta maalumu kwa ajili ya wateja kujisajili na kufanya ubashiri wa michezo inayoendelea mubashara huku kikiwa kimefungwa 'skrini' maalumu za runinga zinazoonyesha michezo mubashara inayochezwa kwa wakati huo na kutoa nafasi kwa wateja kufuatilia matokeo ya mechi hizo.




Meneja Uendeshaji wa Betway Tanzania, Jimmy Masaoe, akiwa katika picha ya pamoja na washindi wa mashindano ya kubashiri yalioendeshwa na Betway wakati wa uzinduzi wa Kituo cha Kushuhudia Michezo cha Dimba la Betway mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

Aidha, kituo hicho kinatoa nafasi kwa wateja kucheza michezo ya kasino na mingine ya ubashiri huku wakipata fursa ya kuuliza maswali, kusajili akaunti mpya, na kufanya ubashiri kwa kutumia simu na kompyuta zilizopo ndani ya kituo. Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi, Meneja Uendeshaji wa Betway Tanzania, Jimmy Masaoe, alisema uzinduzi wa kituo hicho ni sehemu ya juhudi za kampuni hiyo kuongeza thamani katika sekta ya michezo nchini.

"Sisi (Betway) tuna furaha kubwa kuzindua kituo hiki cha kipekee na muhimu kwa mashabiki wa michezo Tanzania kuweza kukutana na kufurahia kwa pamoja na kwenye mazingira ya kuvutia. Hii ni sehemu ya ahadi yetu - kuongeza thamani katika michezo ya kubashiri na sekta ya michezo kwa ujumla kwa sababu kituo hiki kitakuwa kama kitovu cha michezo ambapo mashabiki wataweza kukutana, kutazama michezo, na kufanya ubashiri wao kwa njia bora ambayo haijawahi kutokea hapo awali," alisema.

Akizungumza na wadau wa michezo pamoja na wanahabari waliohudhuria tukio la uzinduzi, Jimmy alisema Betway inafanya kazi kutimiza ahadi zake za kukuza maendeleo ya michezo nchini Tanzania kama ilivyoahidi wakati ikiingia nchini na kuwahakikishia wote kuwa kampuni hiyo itaweza kuwaongoza wateja wake katika kuishi na kuitimiza kauli mbiu ya "Bashiri Kistaarabu" kwa kuwaonyesha wateja wake kwa vitendo.

Michezo

Jumatatu Septemba 13, 2021

Nipashe



Lukaku afunguka ndoto kufunga Stamford

UKURASA 22

# YANGA SASA YASUBIRI KUPINDUA MEZA UGENINI

## ●●●Yakubali kulala dhidi ya Wanigeria, KMKM nayo yaangukia pua kwa Walibya...

**Adam Fungamwango, DAR na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga ya Dar es Salaam na KMKM ya Zanzibar, jana walishindwa kuutumia vema uwanja wa nyumbani baada ya kukubali vipigo katika mechi zao za awali za Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo sasa kujipanga kwa ajili ya kwenda kupindua matokeo 'meza' ugenini kwenye mechi za marudiano mwishoni mwa wiki.

Yanga ambayo iliwakaribisha wageni wao Rivers United ya Nigeria, ilikubali kipigo cha bao 1-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam wakati ndugu zao wa Zanzibar, KMKM wakiwa dimba la Amaan wakiangukia pua kwa mabao 2-0 dhidi ya Al-Ittihad ya Libya.

Kwa matokeo hayo, Yanga sasa inahitaji kupata ushindi kuanzia mabao 2-0 kwenye mechi ya marudiano wakati KMKM yenyewe ikihitaji kushinda kuanzia mabao 3-0 ili kutinga raundi ya kwanza ya michuano hiyo.

Bao lililopeleka simanzi kwa Yanga lilifungwa na Moses Omone dakika ya 51, mpira ukigushwa na wachezaji wawili, kabla ya kumfikia mfugaji aliyeukwamisha nyavuni kwa kichwa. Ilikuwa krosi ya Lookman Binuyo, iliyokwenda kwa Enyiama Kazie ambaye aliupiga kichwa, kabla ya mfungaji hajaumalizia wavuni.

Baada ya bao hilo, Yanga ilionekana kuzinduka kutoka usingizini, lakini mara nyingi pasi zao za mwisho zilikuwa hazifiki kwa walengwa, au wachezaji wao kuwa na papara wanapofika golini.

Yanga ilianza mechi kwa kasi, na iliwachukua sekundi 29 tu kulifikia lango la Rivers United, wakati Yacouba Songne alipoambaa na mpira kwenye wingi ya kushoto, kabla ya kuurudisha nyuma, ukamkuta Zawadi Mauya, akiwa mita zipatazo 30 kutoka langoni, akakandamiza shuti kali lililopita juu la lango.

Baada ya hapo, mpira ulichezwa zaidi katikati ya uwanja, na kwenye dakika ya 19, Yanga nusura iandike bao kwa mkwaju wa faulo uliopigwa kiufundi na Adeyum Selemani, lakini mpira uliparaza nyavu za juu, huku wengine wakidhani kuwa ni bao.

Dakika moja baadaye, Heritier Makambo, aliingia ndani ya eneo la hatari na kuachia shuti la mguu wa kushoto uliompita kipa wa Rivers United Sochima Elum. Wakati kila mmoja akitazamia mpira ukwame wavuni, ulitoka sentimeta chache kwenye lango.

Yacouba, kwa mara nyingine, aliikosesha Yanga bao dakika ya 30, kwa kumegewa pande kutoka kwa Feisal Salum, lakini shuti lake akiwa karibu na goli, lilitoka nje ya lango. Wageni, ambao walikuwa wakifika golini kwa Yanga kwa kuvizia, hatimaye walilitia msukosuko lango la Yanga dakika ya 41, Moses akikosa bao la wazi akiwa na kipa Djigui Diarra, kabla ya kusawazisha makosa yake dakika ya 51 kipindi cha pili.

Yanga iliwatoa Makambo aliyeumia na nafasi yake ikachukuliwa na Yusuph Athumani, Yacouba alitoka na kuingia Ditrim Nchimbi, huku Zawadi Mauya naye akienda nje, Saido Ntibazonkiza akiingia.



Kiungo wa Yanga, Mukoko Tonombe, akimiliki mpira dhidi ya mchezaji wa Rivers United ya Nigeria kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. Yanga ilichapwa bao 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

## Azam FC: Hesabu CAF bado ngumu

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuanza na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Horseed SC ya Somalia, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema hilo haliwapi uhakika wa kusonga mbele katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika na kwamba wanahitaji kupambana zaidi ili kushinda katika mchezo wa marudiano.

Mabao ya Azam katika mchezo huo yalifungwa na Ayoub Lyanga, Idris Mbombo na Lusajo Mwaikenda ambapo walitoka nyuma kwa bao 1-0 na kupindua meza kwa ushindi huo mnono.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Bahati alisema amefurahishwa na matokeo hayo licha ya kuanza kipindi cha kwanza wakiwa chini ila baada ya mapumziko vijana wao walipambana na kupata matokeo hayo chanya.

"Kipindi cha kwanza hatukucheza vizuri ila nawapongeza vijana wangu kwani kipindi cha pili walikuwa na morali na kufanikiwa kupata mabao mawili baada ya kuingia na mpango wetu kwa kutumia ubora na mapungufu yao," alisema Bahati.

Kuhusu mchezo wa marudiano utakaochezwa katika ardhi ya Tanzania tena, alisema ni faida kwao na ana matumaini katika mpira wa kisasa hakuna nyumbani au ugenini, hivyo wanachotakiwa ni kupata matokeo.

"Faida tutakayoipata ni kuto kusafiri, mpira wa kisasa hakuna cha nyumbani wala ugenini kokote unaweza pata matokeo cha kufanya ni kupambana na kuwasisitiza wachezaji kutobweteka na matokeo ya mechi hii," alisema Bahati.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Horseed, Mohammed Hussein, licha ya kupoteza kwa mabao 3-1, amewapongeza wachezaji wake kwa kile walichokionyesha kwani walijua wanacheza na timu kubwa.

"Azam ni timu kubwa na tangu tunatoka Somalia tulijua tunaenda kucheza na timu kubwa na niwapongeze vijana wangu kwa kucheza vizuri licha ya kwamba tulifungwa," alisema Hussein.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042